

Njia Za Kupata

FEDHA

Bila Jasho



*Elimu ya fedha isiyopatikana
Chuo Kikuu*

CHAGUA KUFANYA KAZI MIAKA YOTE AU KULA BATA MIAKA YOTE

Venerando J Milinga

NJIA ZA KUPATA FEDHA BILA JASHO

**@Michese Publishers Company,
Mtaa wa Muungano, Michese,
Dodoma Tanzania.
*Simu 0767285417 /Milinga206@gmail.com***

All rights reserved for Michese Publishers Company

ISBN: 978-9987-9797-4-5

TAHADHARI:

Haki zote za kitabu hiki zimehidhiwa kisheria. Hairuhusiwi kunakili au kutoa nakala yake (photocopy) wala kukisambaza bila idhini ya Mwandishi au Msambazaji. Vyombo vya habari, magazeti, redio, televisheni na mitandao ya kijamii hawaruhusiwi kutoa sehemu ndogo ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi au wasambazaji wa kitabu hiki. Hata hivyo, waandishi wengine wa vitabu vyenye mwelekeo unaofanana na hiki wanaruhusiwa kufanya rejea tu kutoka kwenye kitabu hiki na siyo vinginevyo.

YALIYOMO

SHUKRANI.....	5
SURA YA 1.....	6
Fedha ni nini?	6
SURA YA 2	10
Ukweli Uliofichika Kuhusu Fedha.....	10
SURA YA 3	16
Mitazamo Hasi na Potofu kuhusu Fedha Inayofanya watu Wafanye Kazi Bila Kupumzika Miaka Yote.....	17
SURA YA 4	20
Nidhamu ya Fedha	21
SURA YA 5	26
Bila Nidhamu ya Fedha Utafanya kazi milele.	26
SURA YA 6.....	33
Tengeneza “Kipato-Lala” Kutoka “Kipato- Kazi”	33
SURA YA 7	36
Njia Nne za Kupata Kipato Duniani Kote.....	36
SURA YA 8	58

Miradi ya Kuepuka Kufanya Uzeeni	58
SURA YA 9	68
Miradi 15 itakakuyoleta Fedha Bila Jasho	68
SURA YA 10	107
Kwa nini Watu Hustaaifu Kazi	107
SURA YA 11	111
Maana ya Kustaafu	111
SURA YA 12	113
Uhuru wa Kifedha ni nini?.....	113
SURA YA 13	115
Misingi 3 ya Kupata Fedha Bila Jasho	116
SURA YA 14	121
Una Ndoto Gani Utimizapo miaka 60?	121
SURA YA 15	127
Mithali 60 za Mr. Milinga	127

SHUKRANI

Namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuandika kitabu hiki chenye mawazo ya kuhamasisha msomaji kuchukua hatua za maendeleo yake binafsi. Maendeleo ya watu yanayotafutwa yapo humu kitabuni. Yamefafanuliwa vyema.

Ninamshukuru mchapaji wa kitabu hiki kwa kutengeneza ukurasa wa sura ya mbele na wa nyuma (Front and back cover) na kukifanya kitabu kiwe na mwonekano mzuri kukuvutia kusoma kuchoka.

Aidha, nawashukuru wasomaji wangu wote walionitia hamasa ya kuandika kitabi hiki na vingine vya hamasa ya maendeleo. Hakika, Wasomaji wamekuwa chachu ya kunihamasisha kuandika vitabu zaidi na zaidi mwaka hadi mwaka.

Mwenyezi Mungu awajalie wasomaji wote haja za mioyo yenu kifedha, kiuchumi na kiroho.

SURA YA 1

Fedha ninini?

Fedhani Chombo kilichohalalishwa na serikali halali ya wananchi nawananchi wote wamekubali chombo hicho kitumike kwenye kubadilishana Bidhaa au Huduma sokoni.

Sokoni ni mahali popote ambapo **mnunuzi** na **muuzaji** wa bidhaa au huduma hukutana na kubadilishana bidhaa zao au huduma zao kwa kutumia fedha au pesa. Wanabadilishana kwa fedha.

Fedhalazima iwe nathamani inayotambulika na kulindwa kisheria ndani ya nchi husika ili kuwalinda watumiaji wasiangukie kwenye mikono ya waharifu wanaoweza kuchapisha fedha bandia na kuziingiza sokoni.

Fedha bandia (noti fake) ni makaratasi yaliyochapishwa na wajanja wajanja wa mijini kwa kutumia mifumo ambayo haijaidhinishwa na Benki Kuu ya Taifa.

Fedha bandia huharibu uchumi wa mtu na taifa. Kwa sababu zinakuwa hazijapitia mfumo rasmi

wa Benki Kuu ya Taifa ili kupewa uhalali kisheria kutumika kama nyenzo ya kubadilishana bidhaa au huduma.

Fedha lazima iwe na uwezo wa kumsaidia mtu kutatua matatizo yanayoweza kumkabili wakati wowote. Ndiyo maana watu huweka akiba ya fedha.

Sheria za fedha zinawalinda wawekaji wa akiba ili fedha zao zibaki salama na zifae muda mwafaka zinapohitajika kwa aliyeweka akiba. Hapa ndipo linapokuja suala la mabenki ya biashara, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Mifuko ya Dhamanana Benki Kuu ya Taifa. Taasisi hizo hutumika kulinda thamani ya fedha kwa miaka mingi ijayo.

Fedha tunayotumia Tanzania ni kitu kilichotengenezwa kwa kalatasi maalum au madini maalum na kuitwa “**noti**” au “**sarafu**”.

Tanzania tuna aina mbili tu ya fedha iliyohalalishwa rasmi kisheria na Benki Kuu ya nchi yaani NOTI na SARAFU. Tuna noti za 10,000; 5,000; 2,000; 1,000. Upande wa Sarafu tuna sarafu ya 500, 200 na 100.

Sarafu hizo hutengenezwa kwa kutumia madini ya chuma, aluminiamu au shaba. Noti zetu

hutengenezwa kwa kutumia pamba, katani, rangi mbalimbali, maandishi na alama mbalimbali za taifa.

Kama nilivyofafanua awali, chombo pekee chenye mamlaka ya kuhalalisha **notinasarafuzitumike** nchini ni Benki Kuu ya Tanzania. Noti na sarafu zote ambazo hazijahalalishwa na Benki Kuu ya Tanzania huitwa fedha batili au noti bandia (Fake money) na hazitakiwi kutumika kwenye kununua huduma au bidhaa sokoni.

Ni kosa kisheria kote duniani kutumia noti au sarafu ambazo hazikuidhinishwa na Benki Kuu ya nchi husika. Ukikamatwa unatumia noti bandia utachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwemo kufungwa na kufilisiwa.

Mwenye Mamlaka ya kisheriaanayeruhusiwa kusambaza noti na sarafu za fedha Tanzania ili zitumiwe na wananchi kubadilishana bidhaa au huduma kila siku sokoni ni Benki Kuu ya Taifa tu.

Benki Kuu ya Taifa husambaza noti na sarafu kwa wananchi kupitia Mabenki ya biashara yote kama vile NMB, CRDB, NBC, n.k na wananchi huzipata noti za fedha hizo kwa njia ya: ***mishahara, mikopo,***

gawio(dividends),Pensheni, Kiinua Mgongo, Misaada, tenda,n.kili wananchi huzitumiafedha hizo kupitia bidhaa au huduma wanazohitaji.

Fedha au noti hizo wananchi huzirudisha benki za biashara tena kupitia kuweka akiba benki na kutoka kwenye benki za biashara noti hizo hurudishwa tena Benki Kuu na huo ndiyo huitwa mzunguko wa fedha nchini au katika jamii.

Mzunguko wa fedha unapokuwa mdogo nchini maana yake ni kwamba Mabenki ya biashara yamepunguza kutoa mikopo kwa wananchi au serikali imeacha kuajiri watumishi wapya au haijapandisha mishahara ya wafanyakazi. Sababu hizo hupunguza mzunguko wa fedha nyingi kwa watu wengi na husababisha hali ya upatikanaji fedha mtaani kuwa ngumu.

SURA YA 2

Ukweli Uliofichika Kuhusu Fedha

Watu wengi hawaelewifedha hutoka wapi hadi kuwafikiakama nilivyomaliza kufafanua kwenye sura iliyopita. Hali hii ya kutojua fedha hutoka wapi huwafanya watu kuzeeka kazini bila kupumzika.

Wapo wanaodhani fedha huchimbwa ardhini. Wapo wanaodhani noti au sarafu tunazotumia Tanzania huchapishwa na matajiri wakubwa.

Kuna maandiko matakatifu yanasema *“fedha na dhahabu ni mali ya Mungu”*. Kutokana na maandiko hayo; wapo wanaoamini kuwa bila Mungu mwenyewe hawawezi kupata fedha. Wanashindwa kuelewa huyo Mungu analetaje fedha wakati yeye yuko Mbinguni? Wengine hushikilia andiko moja na kusahau andiko lingine kuhusu fedha.

Wapo wanaoamini kuwa “Mashetani” ndiyo yanayotoa fedha kwa watu. Kuthibitisha hilo ndiyo maana utaona watu wanahangaika na kutoa kafara au matambiko ya kutafuta mali na

fedha. Kuna mitazamo mingi sana katika jamii linapokuja suala la fedha.

Je, wewe unajua fedha hutoka wapi mpaka zikufikie ulipo?

Majawabu yafuatayo yatakushangaza sana. Hivi ndivyo fedha hupatikana kwa kila mtu Tanzania:

1. Fedha ni matokeo (results) ya kazi yako au jasho lako. Fedha ni matunda ya kazi za mikono yako. Ukifanya kazi yenye ahadi ya malipo lazima ulipwe pesa kwa kazi hiyo. Baada ya kazi ni fedha.
2. Fedha nifidia ya jasho lako ulilotoa wakati unafanya kazi fulani yenye thamani sawa na fedha hiyo uliyoahidiwa kupewa ukifanya kazi.
3. Fedha ni fidia ya damu yako uliyotumia kufanya kazi ili upate fedha hiyo. Bila damu mwilini mwako hungeweza kufanya kazi hiyo.
4. Fedha nikitu unachopewa na mwenye nacho ili ukitumie kufanya manunuzi ya vitu ambavyo bila fedha huwezi kuvipata.

5. Fedha ni alama ya utamaduni wetu Tanzania. Ukiwa na fedha ya Tanzania ni ishara kuwa wewe ni Mtanzania au umetokea Tanzania. Mataifa yote hutumia fedha zake kutangaza utamaduni waowa taifa.
6. Fedha ni zawadi au tuzo (award) apewayo mtu baada ya kutatua matatizo fulani ya watu wengine katika jamii. Ukitatua matatizo mengi kwa watu wengi ndivyo unavyopata fedha nyingi.
7. Fedha ni chombo unachopewa ili uweze kukitumia kurahisisha kubadilishana bidhaa na huduma sokoni (Mnunuzi na Muuzaji).
8. “Fedha hutoka kwaMungu” kupitiaSerikali halali ya nchi. Serikali husambaza fedha kwa watu kwa niaba ya Mungu mwenyewe. Mataifa yote duniani husambaza fedhakwa wananchi kwa niaba ya Mungu ili watu wake Mungu waitumie fedha hiyo kuboresha maisha yao.
9. Fedha nimalipo halali kwa mtu aliyefanya kazi au huduma halali. Bila kufanya kazi au kutoa huduma unaweza usipate fedha kabisa.

10. Watu pia hupata fedha kutokana na sadaka zitolewazo kutoka kwa wasamaria wema kusaidia wasio na uwezo au wenye uhitaji.
11. Fedha pia huweza kupatikana kutokana na rambirambi za kufariji waliopatwa na misiba katika jamii. Ikitolewa kama rambi rambi nayo ni fedha halali kwa matumizi halali ya kwenye msiba huo.
12. Fedha ni kipimo cha utajiri wa mtu, familia, ukoo au taifa. Ukiwa na fedha nyingi ni taswira kuwa wewe ni tajiri. Ukiwa na fedha kidogo inatafsiriwa kuwa u maskini sana.

Maneno yaliyoko kwenye kioo yanaashiria kutokujua fedha ni nini na hutoka wapi. Kuna watu hawajui pesa zinatoka wapi



Je, Kazi na Fedha ni Kipi Huleta Heshima?

Ukweli ni kwamba, Kinachomletea heshima mwanadamu siyo fedha bali kazi kwa sababu fedha huja kwa mtu kutokana na kazi au uwekezaji alioufanya.

Hata katika jamii zetu nyingi, kama huna kazi ya kukupatia fedha utakosa heshima. Msichana anayechumbiwa humdharau kijana ambaye atakuja kwake kutafuta amchumbie endapo kijana huyo hana kazi.

Jambo ambalo ataulizwa kwanza ni “unafanya kazi gani?” hilo ndilo swali la siku zote kwa vijana wanapochumbiana. Kazi ndiyo huleta fedha na siyo fedha ndiyo ilete fedha. Fedha haileti fedha bali kazi ndiyo huleta fedha.

Kama hauna kazi yenye staha (decent job or work) huwezi kuwa na fedha za kukupa heshima mtaani au mbele ya jamii yako.

Hata kama utakuwa na fedha nyingi lakini jamii ikajua kuwa fedha hiyo haikupatikana kwa kufanya kazi halali na inayokubalika katika jamii kisheria utakosa heshima mtaani tu.

Heshima yako itashuka tu. Jamii zetu tangu zamani ziliwaheshimu watu wanaofanya kazi. Heshima hakupewa mtu kwa sababu ya fedha zake bali kazi yake. Kinacholeta heshima ni kazi siyo noti.

Kazi ya mtu ndiyo inapaswa kuheshimiwa na siyo fedha. Heshimu kazi yako siyo fedha zako. Heshimu kazi za wengine. Usidharau kazi ya mtu. Usidharau kazi yoyote halali kisheria inayoleta fedha.

Chanzo cha fedha ni kazi. Ujira wa kazi ni fedha. Hivyo, fedha ni matokeo ya kufanya kazi.

Matatizo mengi huanza tu pale watu wanapopenda fedha badala ya kazi. Ukipenda fedha utakuwa mtumwa wa fedha.

Tafuta kuwa mtumwa wa kazi ili baadaye uwe mfalme au mtawala wa fedha.

Ukipenda kazi yako utafanya kazi yako bila kulalamika wala kukata tamaa. Ukijiheshimu na fedha itakuheshimu.

Wanakosea sana wasioheshimu kazi badala yake wanaheshimu fedha. Wanakosea sana wanaopenda fedha badala ya kazi. Wanakosea sana wanaosema fedha ni kila kitu maishani mwao badala ya kuona kuwa kufanya kazi ndiyo huleta kila kitu.

Watapata fedheha sana siku watakapokosa fedha watu hao. Ndugu msomaji, unapaswa kuwa na aibu sana unapokosa kazi siyo unapokosa pesa.

Mithali za Mr. Milinga: Usimwombe Mungu fedha, mwombe akupe kazi iletayo fedha.

SURA YA 3

Mitazamo Hasi na Potofu kuhusu Fedha Inayofanya watu Wafanye Kazi Bila Kupumzika Miaka Yote

Watu wengi bado wana mitazamo hasi (negative mindsets or wrong perception) kuhusu pesa na ndiyo chanzo kikubwa cha wengi kutofanikiwa. Ukitaka ufanikiwe lazima uondokane na fikra potofu kama hizo. Ifuatayo ni orodha ya fikra hasi kuhusu pesa au fedha katika nchi yetu:

1. Wapo wanaosema “fedha ni ibilisi”. Kama ilivyofafanuliwa awali, ukweli ni kwamba fedha siyo ibilisi. Moyo wa mtu ndiyo hujaa ibilisi nasiyo kwamba fedha (noti au sarafu) imejaa ibilisi.
2. Wengine husema kuwa Pesa huleta Heshima. Ukweli ni kwamba Heshima huletwa na ile kazi afanyayo mtu kama nilivyofafanua mapema. Madaraka au mamlaka aliyonayo mtu ndivyo huleta heshimanasiyo fedha yenyewe kama ilivyo noti au sarafu. Kadri unavyokua na Ukubwa wa Madaraka, Cheo, Uwezo na Mamlaka ndivyo unazidi kuwa na fedha kubwa zaidi.

3. Wapo watu husema “mtu akipata fedha anachanganyikiwa”. Ukweli ni kwamba mtu akikosa pesa pia anachanganyikiwa. Hivyo, *kinachowachanganya watu siyo wingi wa fedha* au kukosa fedha bali ni misongo mingi ya mawazo inayokuja kwa mtu baada ya kupata fedha nyingi au anapokosa fedha za kutosha mahitaji ayatakayo.
4. Wapo watu husema “Fedha nyingi” hutoka kwa majini au mashetani au freemason. Huo ni mtazamo potofu sana. Ukweli ni kwamba majini au mashetani hayapo kwenye fedha (noti au sarafu) zenyewe bali mashetani yapo kwenye fikra, akili au moyo wa mtu mwenyewe siyo kwenye fedha zenyewe.
5. Watu wengine wanaamini kwamba *“fedha ni chanzo cha kila Uovu”* wanasahau tafasiri sahihi ni kuwa “kupenda fedha” ndiyo “chanzo kikubwa cha maovu ya kila aina” siyo fedha yenyewe kama ilivyo katika uhalisia wake wa noti au sarafu.
6. Wapo wanaoamini kwamba wataenda peponi au mbinguni kwa sababu wao siyo matajiri. Ni kweli kwamba kuwa na utajiri

siyo tiketi ya kwenda mbinguni. Lakini pia umaskini nao siyo tiketi ya kwenda mbinguni. Tiketi ya kwenda mbinguni au peponi siyo fedha nyingi wala umaskini mwingi ni usafi mwingi wa moyo wako. Tafuta fedha nyingi pia acha maovu yako hakika utaingia peponi.

7. Wapo wenye mtazamo potofu kuwa “fedha ni sabuni ya roho”. Wapo pia wasemao pesa ni “jawabu la mambo yote” bila kuelewa tafsiri yake. Ukweli kwamba fedha ikitumika kutatua matatizo ya watu ndipo inakuwa sabuni ya roho na jawabu la mambo yote yanayowezezana kutatuliwa kwa fedha. Je, unatafuta fedha ili utatue matatizo ya watu?

8. Je, unatafuta pesa ili uitumie kutatua matatizo yako na jamii yako? Matendo mema kwa watu unapopata fedha ndiyo huonekana sabuni ya roho. Fedha uliyonayo haitakuwa na maana yoyote kama haitumiki kutatua matatizo yako na jamii yako. Weka mikakati yako katika kutatua matatizo ya jamii yako ndipo fedha itakuwa ya maana sana kwako na jamii yako yote. Ndipo fedha itaitwa sabuni ya roho na jawabu la mambo yote.

Mf: Ukipata Mil. 150 utafanyia nini?



Zoezi la Vitendo:

- 1. Hebu jaribu kuwaza; kama ukipata shilingi milioni mia moja na hamsini (150,000,000) utazitumiaje mpaka ziishe zote?*
- 2. Ni biashara gani au miradi gani unapanga ufanye kwa pesa hiyo ambayo una uhakika kwamba ukiwekeza fedha hiyo kwenye utapata kipato chakutosha mahitaji yako kila mwezi(monthly bills) kwa maisha yako yote yaliyosalia?*

Mithali za Mr. Milinga:

Mungu Hubariki Kazi za Mikono, Tumia Mikono Yako Kufanya Kazi Nyingi Upate Fedha nyingi.

SURA YA 4

Nidhamu ya Fedha

Bila Nidhamu ya Fedha Utafanya kazi milele.

Watu wote waliofanikiwa duniani walijenga utamaduni wa maisha yenye nidhamu kwenye fedha zao kila siku. Waliofanikiwa wote wanaeleza kwamba bila kujenga utamaduni wa nidhamu ya fedha hakuna kufanikiwa kifedha kamwe.

Matajiri wote waliofanikiwa walifanya juhudi kujifunza kuweka nidhamu ya fedha. Maelezo yafuatayo kuhusu nidhamu katika fedha yatakuwezesha kujenga nidhamu kubwa ya Fedha:

Nidhamu ya fedha ni nini?

- Ni uwezo wa kupanga na kutekeleza ulichopanga kufanya Kabla ya kupata pesa na baada ya kupata pesa. Ni uwezo wa akili ya mtu kutokuyumbishwa na upepo wa mahitaji yasiyokuwa kwenye mpango wa bajeti mara tu anapopata pesa.

- Ni msimamo wa mtu *kuazimia kutotumia pesa vibaya* au kutotumia pesa tofauti na mipango yake aliyojiwekea ili aweze kutimiza ndoto za mipango yake ya mafanikio aliyopanga kuifikia muda fulani ujao.
- Nidhamu ya fedha *ni utamaduni unaojengeka ndani ya mtu* hatua kwa hatua mwaka hadi mwaka tangu akiwa mtoto mdogo na hudhihirika kivitendo akiwa mtu mzima atakapoanza kupata fedha zake mwenyewe.
- Ni utamaduni unaomwezesha mtu kujizuia kufanya matumizi ambayo hakuyapanga mapema kabla ya kupata pesa.
- Nidhamu ya fedha ni **udhibiti** wa ndani ya mtu mwenyewe (Self internal controls) anaokuwa nao mtu unaomwezesha binafsi kuheshimu fedha anazopata na kuzitumia kama alivyopanga tu.
- Nidhamu ya fedha ni **hulka** aliyonayo mtu ndani yake inayomwezesha kujilinda na kujitambua kiasi kwamba hawezi kupelekeshwa na upepo, mihemko na

kufuata mkumbo kufanya matumizi ya fedha zake.

- Nidhamu ya fedha ni **tabia** inayoonekana wazi kwa mtu kutii na kuheshimu bajeti yake binafsi, bajeti ya familia au taasisi, kuanzia awapo na fedha ndogo au akiwa na fedha nyingi sana kuanzia ngazi ya familia hadi ngazi za juu za taasisi zenye fedha nyingi.
- Nidhamu ya fedha ni uwezo wa **kujitawala kihisia na kifikra** na kuepuka matumizi ambayo hayajakubaliwa kutumika hivyo.
- Nidhamu ya fedha ni ujasiri wa **kukataa** kutumia fedha kwenye mipango ambayo haikuwepo awali wakati safari ya kutafuta fedha ilipoanza.
- Nidhamu ya fedha ni kutafuta mafanikio hatua kwa hatua na siyo kutafuta mafanikio ya haraka yasiyotokana na mipango wala kazi za kueleweka. Mtu yeyote anayetafuta mafanikio makubwa haraka haraka huyo hana nidhamu ya fedha.
- Nidhamu ya fedha haipatikani kwa kusoma sana shuleni au chuoni bali ni malezi bora

ya tangu utotoni kuwa na nidhamu ya fedha zote anazopata kwa jasho lake.

- Wazazi tunao wajibu mkubwa kufundisha watoto kuheshimu mipango na bajeti zao ili wawe na nidhamu ya fedha ambayo ndiyo msingi mkuu wa mafanikio maishani mwao baadaye.

ZOEZI:

1. **Andika Miradi yote utakayoifanya siku ukipata shilingi 60,000,000 au 80,000,000 au 150,000,000?**
2. **Hiyo miradi utakayofanya unataka kwa mwezi ikuingizie shilingi ngapi na kwa nini?**
3. **Miradi hiyo utakayofanya unataka idumu kwa miaka mingapi baada ya Kustaafu?**
4. **Ndoto yako ukistaafu ni kupata shilingi ngapi kwa mwezi?**

Kuna watumishi wa umma wakistaafu hulipwa fedha zaidi ya shilingi milioni mia moja kutegemeana na vyeo au ukubwa wa mishahara na idadi ya miezi waliyokaa kazini.

Watumishi wa umma wengi hufanya makosa mengi wanapostaafu na kujikuta wametumia fedha zao vibaya na kuanza kujutia fedha hizo lakini wakiwa hawawezi tena kuzirudisha. Ni matokeo ya ukosefu wa nidhamu ya fedha.

Kama wewe ni mtumishi wa umma na unakaribia kustaafu mwaka huu jitahidi kupanga mipango inayolingana na matarajio yako ya Kiinua Mgongo.

Aidha, ili kujua utalipwa kiasi gani tembelea ofisi za Mfuko (NSSF au PSSSF) upatiwe mahesabu tarajiwa ya mafao yako ili uanze kujipanga kutekeleza miradi kwa nidhamu ya hali ya juu kama ilivyoelezwa kwenye kitabu hiki.

SURA YA 5

Bila Nidhamu ya Fedha Utafanya kazi milele.

(Nidhamu ya Fedha za Mshahara, Mikopo na Kiinua Mgongo)

Mbinu za Kuwa na Nidhamu ya Fedha.

Miaka 15 iliyopita nimefanya kazi ya kuhudumia wastaafu nakushauri sana wafanyakazi kuhusu masuala ya ya Hifadhi ya Jamii, Kiinua Mgongo, Pensheni na Uwekezaji wenye tija.

Kwa kipindi chote hicho nimeona wafanyakazi wengi wakistaafu na kulipwa fedha katika viwango tofauti na wengi wakishindwa kuzitumia fedha zao vema baada ya kustaafu.

Nimeona wafanyakazi wengi wakichanganyikiwa. Nimeona wengine wakifariki mapema mara tu baada ya kulipwa fedha za mafao yao ya utumishi wao.

Nimeshuhudia wengi wakishindwa kuamini kilichotokea mara tu wanapoishiwa fedha walizolipwa za mafao yao. Fedha zinayeyuka ghafla. Naam Fedha zinawaishia haraka sana

kuliko walivyodhani kabla ya kustaafu. Kuna tatizo kubwa.

Pia nimeshuhudia wafanyakazi wengi mishahara yao ikionekana haitoshi. Mwezi hadi mwezi wanalalamika. Wengi fedha zao za mishahara huisha haraka kuliko walivyodhani. Mishahara inaisha haraka sana hata kabla ya wiki tatu kwisha. Tatizo.

Nimeona wafanyabiashara wengi wakichukua mikopo kwenye mabanki na taasisi nyingi za mikopo. Hata hivyo, wengi wamekuwa wakishindwa kutimiza malengo ya mikopo yao. Fedha zinwaishia kabla ya kufanya lolote au kabla ya kutimiza ndoto zake. Kuna shida kubwa sana.

Nimeshuhudia watu wengi wakichukua mikopo Benki au SACCOS na baadaye wengi kujikuta wamefilisiwa mali zao kwa kushindwa kurejesha mikopo waliyopewa na benki au SACCOS.

Katika kipindi hicho cha miaka 15 ya kufanya kazi nimeshuhudia wengi waliopata fedha za kiinua mgongo, mkopo, mishahara au mauzo makubwa ya biashara wakijikuta fedha zote zimewaisha bila kutimiza lengo hata moja walilokusudia. kuna tatizo sana mahali fulani kwenye jamii yetu.

Je, matatizo hayo husababishwa ya fedha kuyeyuka huletwa na nini?

Katika sura hii, nitakupitisha katika mambo kadhaa yatakayokuwezesha kupata maarifa na mbinu zitakazokusaidia kuwa na nidhamu ya fedha. Maarifa hayo ni haya yafuatayo:

1. Panga miradi ya kufanya kabla ya kupata pesa unayotarajia kupata. Usisubiri pesa imeshafika mkononi mwako ndipo uanze kupanga bajeti. Usipopanga bajeti kabla hujapata pesa utazitumia hovyoya bila nidhamu.
2. Panga kutumia asilimia 10 tu kwenye mambo yasiyohusiana na mradi uliokusudia. Halafu asilimia 90 yote hakikisha inaishia kwenye miradi uliyopanga kutekeleza.

Ndugu, jamaa na marafiki utakaowasaidia hakikisha kuwa hautazidisha asilimia 10 ya Mkopo wako, kiinua mgongo chako, mshahara wako, n.k. Kama ni kutoa sadaka za kawaida kanisani au mskitini, usitoe sadaka kwa mihemko ya wahubiri bali jipangie kiasi utakacho.

3. Mara tu unapopata pesa anza mara moja kutekeleza miradi yako bila kungoja ngoja

wala kuziacha fedha benki eti zitulie kwanza. Usianze kusitasita au kuduwaa na kushangaa. Anza kazi mara moja. Elekeza fedha zote kutekeleza ulichopanga kufanya ulipokuwa haujapata pesa. Epuka kuahirisha tena.

4. Mara tu fedha inapopatikana mpe taarifa mwenzako wa ndoa au watoto wako. Mpe taarifa kwamba fedha uliyokuwa unaitarajia imeingia. Kisha miradi mliyopanga pamoja anzeni kutekeleza mara moja. Usimwambie mtu asiyehusika kuhusu fedha uliyopata.
5. Kwa upande wa mshahara; Kama ungependa kuwa na nidhamu ya fedha za mshahara, hakikisha kila mwezi unapopata mshahara wako unatekeleza jambo ulilojipangia kufanya mwanzoni mwa mwezi. Hakikisha kuwa ulichopanga umekitekeleza. Ukifanya hivyo, uzeeni utainjoi sana wewe na wajukuu zako. Jenga nidhamu ya mshahara wako mwezi hadi mwezi, utashangaa miaka 5 hadi 10 tu wewe ni tajiri hapo mtaani kwako.
6. Mfanyakazi uliyeajiriwa; hakikisha unaweka Kiapo au azimio moyoni mwako kwamba “fedha zote nitakazopata mwezi ujao nitazitumia kwenye mipango niliyoazimia tu”.

Bila kuweka kiapo na kukiheshimu utashitukia fedha zimeisha bila kujua zimeenda wapi. Utaishia kulalamika kwamba mbona fedha zinaisha haraka? Utalaumu kila mtu unayekutana naye.

7. Mfanyakazi unayekaribia kustaafu; hakikisha kuwa unapokaribia kustaafu panga miradi utakayofanya ukistaafu. Panga miradi isiyozidi 2 au 3 kulingana na fedha unayotarajia. Chagua miradi itakayokuwezesha kupata pesa kwa kipindi kirefu bila kutokwa jasho sana.
8. Ukilipwa Kiinua Mgongo baada ya kustaafu, epuka kutumia pesa yako yote kwenye miradi ya ghafla ambayo hukuifanyia upembuzi mapema. Epuka kwenda kwa kila mtu kuomba akupe ushauri wa kitu cha kufanya. Waepuke walimu wa mtaani watakaokwambia hiki au kile kinalipa sana. Usifanye mradi ambao kuufanyia uchunguzi na haukushirikisha mwenzako wa ndoa.
9. Usifanye biashara zenye ahadi ya kupata pesa nyingi au utajiri waharaka (Avoid get rich quick schemes). Utajuta kufanya hivyo huku fedha imeshakutoka.

10. Unapopata fedha nyingi (kuanzia shs 1,000,000 na kuendelea) epuka kutaka kila mtu ajue kuwa umepata pesa. Usikubali kusaidia kila mtu kwenye ukoo wako au kijiji chako. Fedha ya kiinua Mgongo au mkopo wako siyo za kusaidia kila mtu katika ukoo wako. Tumia kiinua mgongo chako au Mshahara au mkopo wako kufanya mradi sahihi uliokusudia. Watu wenye uhitaji hawataisha katika jamii.

11. Mara tu unapopata fedha; iwe ya mkopo, mshahara, ujira, faida au kiinua mgongo; epuka kukopesha marafiki zako. Wengi wakijua kuwa umepata mkopo au kiinua mgongo watakuja kukuomba uwaazime fedha. Ukiwapa tu ujue kuwa ni kama umegawa pesa hiyo. Marafiki na ndugu mara nyingi huchukulia mkopo kama pesa ya bure wamepatiwa. Kama ni lazima kumpa mkopo mtu au rafiki au ndugu mpatie kiasi ambacho hakitakuumiza moyo endapo atashindwa kukurejeshea.

Wengine huona mkopo kama msaada au hisani. Ndugu na marafiki wengi hawako tayari kurejesha pesa ya mkopo hasa kama aliyetoa mkopo ni ndugu/rafiki.

12. Kabla ya kuanza mradi wako wowote soma kitabu cha Biblia katika **Luka Mtakatifu 14:28** panaposema, **“Ni nani akitaka kujenga haketi kwanza na kuhesabu gharama za ujenzi ili asije akachekwa kwa kushindwa kukamilisha....?”** Fanya hesabu na upembuzi wa kutosha kuhusu mradi unaoutaka kuufanya. Usikurupuke kufanya biashara au miradi ambayo haitakuwa uendelevu na uhakika kwa kipindi kirefu.
13. Kama unataka uwe na nidhamu ya fedha; Mwanaume epuka mitego ya warembo, watoto wa kike wabichi, vimwana, totoz, mabeibi, nk. Kama unataka kuwa na nidhamu ya pesa zako tulia na mkeo au mumeo. Tosheka na uliyenaye tu. Warembo duniani hawataisha. Mama wanaume watanashati hawaishi duniani. Pesa zitayeyukia usikokujua. Utakuwa Mwenye fedheha kuu.
14. Mwanamke tosheka na mpenzi mume wako mmoja. Epuka mahusiano na waume za watu kwa nia ya kuwachuna pesa zao. Aidha, achana na ulimbukeni wa kuingia mahusiano na vijana wa kiume wenye umri mdogo. Utamaliza fedha zako bila kuelewa zilikoishia.

SURA YA 6

Tengeneza “Kipato-Lala” Kutoka “Kipato-Kazi”

(How to Create Passive Income from Active Income)

Katika sura hii nitafafanua aina mbili za Vyanzo vya mapato vitokanavyo na njia nne za kupata mapato duniani kote. Ukitengeneza kipato-lala ndipo utaweza kula bata milele. Vinginevyo utafanya kazi milele hadi siku ya kulala kaburini.

Kipato cha aina ya Kwanza; ni “kipato-kazi” (Active Income). Kipato hicho ili kipatikane lazima kufanya kazindipo upate mkate wako. Bila jasho kukutoka hupati fedha. Bila kushughulika kwanza hupati malipo.

Kipato hiki kwenye jedwali hapo chini (linalohusu vyanzo vya mapato duniani) lipo kwenye upande wa kushoto wa jedwali hilo. Kipato-kazi hupatikana kwa mtu ama kwa kuajiriwa au kujiajiri.

Hivyo, kipato-kazi hupatikana kwanjia mbili ambazo ni ama kuajiriwa au kujiajiri.

Kipato cha aina ya Pili; ni kipato-lala au *Passive Income*. Hiki ni kipato apatacho mtu bila kulazimika kwenda kazini **tena** kila siku.

Kipato hiki hupatikana baada ya juhudi za muda mrefu za kuwekeza kwenye mifumo endelevu kwa lengo la kupata kipato kwa muda mrefu ujao.

Watu wote waliofanikiwa walipigania kuwa na kipato kama hiki ambacho hupatikana bila kutokwa jasho kila siku.

Waliofanikiwa kifedha walitengeneza kipato endelevu baada ya kuvipiga vita vilivyo vizuri na mwendo wakaumaliza na kuanza kula bila jasho.

Mara nyingi kutengeneza kipato-kazi huwachukua muda mrefu sana watu wengi. Nchi nyingi za Ulaya na Amerika watu huanza kupata kipato cha aina hii wakiwa na umri wa miaka 40.

Ndiyo maana ya usemi wa wengi kwenye nchi hizo kusema kwamba maisha huanza ukiwa na umri wa miaka 40 au “Life starts at Forty”.

Kwa nchi zetu nyingi Afrika maisha ya kula pesa za bila jasho huanzia miaka 50 au 60 kwa walio

wengi. Kwa hiyo Afrika maisha huanzia umri wa miaka 60 (in Tanzania life starts at 60 not at 40).

Hata hivyo, watu wengi wakiipata elimu hii naamini hawatasubiri umri wa uzeeni kupata “passive income” yaani kipato endelevu.

Wengi wakipewa elimu hii watatengeneza vyanzo vya mapato mapema ili umri wafikapo umri wa miaka 40 wasiyumbe kifedha na kiuchumi.

Ukianza mapema kuitengenezamiundombinu au mifumo ya kukuingizia kipato hiki (Passive Income) hautapata shida ya kipato uzeeni mwako. Utakula bata mpaka siku ya mwisho duniani. Hata wajukuu zako watafurahia matunda ya misingi hiyo uliyoweka.

SURA YA 7

Njia Nne za Kupata Kipato Duniani Kote

Kuna njia 4 tu za kupata kipato hapa duniani. Kuna njia 2 za kupata fedha kwa jasho. Na kuna njia 2 nyingine za kupata fedha bila jasho. Kila mtu anaweza kuwa kwenye njia yoyote kati ya hizi 4. Lakini njia za kupata fedha bila jasho zinafaa zaidi kuchukuliwa kwa uzito. Ni chaguo lako tu.

Jedwali lifuatalo ukurasa unaofuata linawakilisha makundi 4 kuonesha vyanzo vinne vya mapato ya fedha kwa watu wote duniani.

Matajiri wengi huwa upande wa kulia mwa jedwali hilo. Na upande huo ndipo matajiri hupatia fedha bila jasho kutokana na walivyojipanga mapema.

Upande wa kushoto mwa jedwali hilo kunaonesha jinsi watu walio wengi hupatia fedha kwa jasho na uchovu. Usipopambana kuhamia upande wa kulia mwa jedwali hilo utaishia kufanya kazi hadi siku ya kufa kwako. Tazama jedwali:

Njia Kuu 4 za Kupata Fedha (AJBW)

A = AJIRIWA	B = Biashara
J = JIAJIRI	W = Wekeza

Kwa watu waliosoma vitabu vya Robert Kiyosaki Mwandishi maarufu duniani; watakuwa wanaelewa mchoro huo hapo juu kwa urahisi.

Upande wa kushoto mwa Jedwali hilo kuna: **A = Ajira** na herufi **J = Jiajiri**.

Upande huu wa kushoto huwakilisha Watu Walioajiriwa na Waliojiajiri. **Kipato Kazi** (Active Income) kipo kushoto. Upande wa kulia mwa jedwali hilo; kuna “**B**” na “**W**”; Hizo huwakilisha **Wafanya Biashara Wakubwa** na **W=Wawekezaji**.

Kwa hiyo Upande wa kulia wa jedwali hilo huwakilisha kundi la watu wanaopata “**kipato lala**” yaani “*Passive Income*”.

Matajiri wakubwa wote na watu wenye busara wengi hupigania kupata kipato kutoka upande wa kushoto mwa jedwali hilo.

Wote waliofanikiwa maishani wanapigania kutengeneza vyanzo vya mapato kutoka kwenye uwekezaji ili wajiweke kwenye upande wa kupata kipato endelevu kwa miaka mingi ijayo.

Changamoto za Kipato-Kazi (Challenges with Active Income)

Watu wote walioajiriwa na waliojajiri hutafuta Kipato-kazi yaani “*Active Income*” na ndiyo maana wanaenda kazini kila siku.

Kwenye Kundi hili aliyeajiriwa na aliyejajiri hawana tofauti sana. Hawawezi kuchekana. Ndiyo maana watu wakasema kwamba “asiyefanya kazi asile”.

Na mheshimiwa mmoja wa Tanzania aliwahi kusema, “asiyefanya kazi asile na asipokula na afe”. Kwa hiyo bila kufanya kazi huwezi kupata kipato hiki. Kazi kwanza kipato baadaye. Aliyejajiri na aliyeajiriwa wote kanuni hii inawahusu.

Kipato chochote kinachotegemewa kuingia mfukoni kwa Kufanya kazi kila siku ndipo mkate wako wa kila siku upatikane ni kipato kisichoaminika na kinaweza kukuaibisha nyakati ambazo hutarajii.

Zifuatazo ni changamoto za Kipato-Kazi:

1. Usipofanya kazi Kipato kinatoweka:

Kipato kazi hutegemea kazi kila siku. Kupata fedha mfukoni mwako au kwenye akaunti zako za benki kila mwezi lazima ufanye kazi. Ukienda likizo ya miezi mitatu, mine, sita, nkipato hicho hukoma kutiririka kwako. Usipoenda kazini mkono wako hauwezi kwenda kinywani. Bila kazi fedha hakuna.

2. Ukiugua Kwa muda mrefu Kipato hukoma.

Kipato-Kazi hukoma kumiminika endapo utaugua kwa muda mrefu bila kwenda kazini. Ndiyo maana kuna msemu usemao “afya ni mali”.

Kwa sababu hiyo nashauri kila mtu kujitahidi kufanya uwekezaji wa fedha yoyote anayopata kwenye biashara zake au mshahara wake kila mwezi.

Wekeza kwenye mifumo au miradi itakayokupatia kipato endelevu (au kipato-lala) hata kama ataugua kwa muda mrefu.

Hoja hii iwe miongoni mwa vitu vinavyokutia msukumo wa kuwekeza. Hoja hii ya kuugua muda mrefu (endapo itatokea) inapaswa kuwa moto wa kukuwasha ndani ya nafsi yako ili uchukue hatua.

3. Ukizeeka Huwezi kupata Kipato tena.

Kama umeajiriwa au umejiajiri ni kwa sababu bado una umri wenye nguvu. Kuna siku utazeeka na nguvu zitakuishia. Kuna siku hutaweza kufanya kazi kwa sababu za uzee. Je, umejipangaje kifedha?

Una rasilimali gani za kukupatia fedha uzeeni. Umeweka mradi gani utakaokupatia fedha uzeeni mwako? Je, utakuwa omba omba wa fedha za matumizi uzeeni au utajitosheleza kifedha?

Mshahara wa mwajiri wako kuna siku utakoma kulipwa kwa sababu za uzee wako.

Kuna siku hutaenda kazini tena. Hata kama umejiajiri kumbuka kuwa kuna siku utazeeka.

Aliyejajiri hawezi kupata pesa mpaka ufanye kazi. Je, utakapozeeka umeweka mipango gani itakayokupatia fedha bila kwenda kazini? Utakula nini uzeeni? Utapata wapi fedha za kukutosha kula uzeeni hadi siku ya kifo chako?

Mshahara wako utakomea siku utakapotimiza umri wa kutoruhusiwa kuajiriwa tena. Umri wa mwisho kuajiriwa kisheria ni miaka 60 kwa sheria za Tanzania. Je, ukitimiza umri huo umejipanga kuishije? Fedha za kutosha mahitaji yako ya uzeeni utazipata wapi mpaka siku yako ya mwisho kuishi duniani? Wekeza zaidi na zaidi ili uwe na fedha zaidi na zaidi uzeeni.

4. Ukiwa na Kipato-Kazi Hupati Muda wa Kutosha “Kula Bata”.

Wapo watu wenye fedha lakini hawana muda. Kuna watu wenye muda mwingi lakini hawana fedha. Wapo walioajiriwa wengi wenye vipato vizuri lakini hawana muda wa kuyafurahia maisha haya. Wapo *bussy* muda wote.

Kuna watu hudhani kujajiri ni kazi nyepesi. Lakini pia kuna watu wanadhani kuwa ukiajiriwa mambo yanakuwa safi sana. Ukweli ni kwamba kuajiriwa au kujajiri vyote huondoa Uhuru wa kuishi upendavyo.

Huwezi kujiamria kufanya upendavyo kisa umejajiri. Huwezi kusema unaamka saa nne asubuhi kisa wewe umejajiri. Uhuru wanaoukosa watu waliojajiri ni mkubwa sana wakati mwingine hata zaidi ya walioajiriwa.

Uhuru haupatikani kwa watu walioajiriwa au waliojajiri. Muda mwingi wapo na kazi kibao (bussy). Hawawezi kupata muda wa kupumzika au kwenda likizo kila wanapotaka. Waliojajiri hawawezi kupata muda wa kutosha “Kula bata” kama wapendavyo. Wakati mwingine hata siku za mwisho wa wiki hawapti muda wa kupumzika wala kuburudika na marafiki zao. Muda wa kustarehe kama wapendavyo hawawezi.

Wafanyakazi walioajiriwa au kujajiri wapo ambao bado wako hatua zakipato-kazi (active income) hawawezi kupata muda wa kuburudika au kwenda kwenye sehemu za starehe bila kuathiri uhai wa kibarua chako. Mara nyingi kazi yoyote inayokulipa fedha nyingi lazima utajikuta kazi hiyo inakuchukulia muda wako wote na hutapata muda wa kupumzika na kufurahia matunda ya kazi zako.

Hata ukipata muda wa kula bata unakuwa ni mwisho wa wiki tu au wakati wa ukipewa likizo

tu. Hiyo ndiyo changamoto ya kuishi kwa kipato-kazi. Huwezi kuwa na muda wa kufarahi na watoto wako au mkeo au mumeo au ndugu zako.

Huwezi kupata muda mrefu wa kufanya ibada zako uzipendazo. da wote uko kazini. Hiki ni kipato chenye kupatikana kwa jasho.

Faida za Kipato-Lala (Benefits of Passive Income):

Hiki ni kipato kinachopatikana hatakama hufanyi kazi wewe binafsi na hata kama umelala tu pesa inaingia kwako.

Ni kipato kinachoendelea kutiririka, kumiminika, kutelemka, kuingia, na kujaa mfukoni mwako siku hadi siku, mwezi hadi mwezi na mwaka hadi mwaka bila kulazimika kwenda kazini.

Uende kazini au usiende kazini fedha inamiminika tu. Hiki ni kipato endelevu (sustainable income) ambacho hakina mwisho. Watu wote wenye busara hukimbilia kutengeneza kipato hicho.

Wenye hatua hii ya kipato wana fedha nyingi na muda mwingi wa kufarahia maisha watakavyo. Wanao muda wa kusafiri wapendako. Wana

uhuru wa kuishi watakavyo. Wanaweza kwenda likizo hata ya mwaka mzima bila kutetereka kifedha.

Wanao muda wa kufarahi na wanafamilia wenzao. Mume ana muda mwingi wa kufarahi na mke wake, watoto wake na ndugu zake. Huu ndiyo uhuru wa kifedha unaotakiwa. Hilo ndilo lengo la kupambana hadi kufikia viwango vya uhuru wa kifedha.

Wote wenye hekima hutazama mbali sana. Wao huwekeza katika miradi itakayowaletea fedhaujanani, uzeeni nahadi kwa watoto wao au wajukuu zao ikiwezekana. Huwekeza kwenye miradi inayoleta fedha kwa muda mrefu. Huwekeza kwa busara sana ili waishi maisha ya furaha baadaye.

Jinsi ya Kutengeneza “Kipato-lala” (How to Create Passive Income)

Kipato hiki, kama nilivyofafanua awali, hutokana na chanzo kilichotengenezwa kwa muda fulani au miaka kadhaa iliyopita na kilitayarishwa ili kiweze kutiririsha fedha kwa mwekezaji kwa kipindi kirefu bila kulazimika kufanya kazi tena kila siku.

Kipato cha aina hii hutokana namiradi endelevu itakayoleta kipato endelevu, biashara endelevu itakayoleta fedha endelevu.

Upande mwingine kipato hiki siyo lazima kitoke kwenye kitegauchumi au mradi bali yaweza kuwa biashara kubwa endelevu inayojiendesha (automated large scale business) yenyewe kwa kutumia wafanyakazi tofauti na wewe mwenyewe ambapo hata kama wewe hautakuwepo duniani biashara hiyo itaendelea kuwepo na kutiririsha fedha kwa waliopo.

Mataifa mengi yaliyopiga hatua kubwa kiuchumi wananchi wake wengi wana biashara kubwa ambazo zinaweza kujiendesha zenyewe chini ya Bodi za uendeshaji bila kulazimika kusimamiwa na mwanzilishi wake. Hii maana yake ni kwamba wananchi wake wamefikia hatua za kuwa na uhuru wa kipato kwa wingi. Ndiyo maana wanaweza kukaa ndani (lockdown) kwa kipindi kirefu bila kufanya kazi na maisha yakaenda vizuri.

Upande wa nchi zetu za Afrika bado kuna wananchi wenye vitu vingi lakini hawana vipato vingi vitokanavyo na hivyo vitu vingi. Watu wengi Afrika hutegemea kazi za kila siku ndipo wapate mkate wa kila siku.

Hili ni tatizo kubwa sana Tanzania na Afrika. Tatizo hili huwafanya watu wasiwe tayari kustaafu kazi. Hawapo tayari kukabidhiana madaraka ya kisiasa kwa sababu madaraka yenyewe waliyonayo wanayatumia kupata kipato.

Wengi Afrika hata Tanzania wapo tayari kufa wakiwa kazini. Hata kama wameshazeeke sana, bado wanaomba kazi. Wanaomba kula badala ya Kura. Kama ingekuwa siyo sheria za kazi, wengi hawangestaafu kabisa.

Zifuatazo ni baadhi ya njia naomba nikushirikishe kama ungependa kuwa na kipato-endelevu maishani mwako unaweza kuzifuata:

1. Tengeneza Mfumo wabiashara kubwa (Establish an Automated Business).

Kama unaweza kuwa namakapuni ya biashara zaidi ya mawili yakaajiri watumishi wanaoendesha makampuni hayo na ukatengeneza mifumo inayojiendesha yenyewe (automated financial systems) hapo utaweza kupata kipato hiki kwenye hizo kampuni.

Watumishi wanaowekwa kwenye mifumo hiyo lazima wawe watu ambao wana uwezo na maadili kifedha. Kama hawana maadili kampuni zako zote zitashindwa kuendelea endapo wewe hutakuwepo.

Hiyo ndiyo changamoto ya makampuni makubwa ya biashara hasa yanayomilikiwa na watu binafsi. Njia pekee ya kutatua tatizo hilo ni kumilikisha watoto wako waendeshe makampuni hayo. Lakini nao pia kama hukuwalea katika misingi ya biashara hiyo hawataweza kuendeleza makampuni yako kwa miaka mingi.

Hakikisha kuwa kuna mifumo ya wamiliki (wewe na watoto wako) kuwa na hisa kwenye makampuni yote na faida ifahamike mgawo wake. Ikiwezekana wafanyakazi nao waingizwe kwenye makampuni yako wawe wanahisa. Hiyo itasaidia kupunguza hujuma za makampuni yako. Ukifanya hivyo unaweza kupata fedha kwa miaka mingi sana hata kama haupo kazini au duniani.

Mfano mzuri wa mifumo ya biashara kubwa inayoleta kipato endelevu au kipato-lala ni Makampuni ya marehemu Mzee Reginald Mengi aliyekuwa anamiliki makampuni mbalimbali ikiwemo Independent Television Limited

(ITV), Radio One Stereo Ltd, The Guardian Ltd, Bonite Bottlers Ltd, nk.

Pamoja na kwamba mzee huyo ameondoka duniani kampuni zake alizoanzisha akiwa hai zinaendelea kufanya kazi na kutiririsha fedha bila kujali yeye yupo hai kazini au alishaondoka duniani. Marehemu Reginald Mengi alitengeneza mfumo wa kampuni za biashara ambazo hunaingiza fedha awepo au asipokuwapo duniani.

2. Amua Kajiriwa na Ufanye Kazi Hadi Utakapostaafu:

Kama utakavyosoma kwenye mithali za Milinga, nimeeleza kuwa kuajiriwa siyo dhambi, lakini kuzeeka au kufa maskini ndilo kosa kubwa kwako.

Kama utachagua kufanya kazi mpaka siku ya kustaafu huo ni uchaguzi wako. Siyo dhambi kuchagua hivyo. Kama mwajiriwa kwenye sekta yoyote ya umma au binafsi kwa sababu ya ujuzi ulionao au kwa sababu ya elimu yako, fanya hivyo kwa bidii maana una fursa ya kupata fedha bila jasho uzeeni utakapostaafu.

Utakula pensheni uzeeni kama utafanya kazi kwa miaka isiyopungua 15 na kuweka akiba kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Huo ni uamuzi wako. Asikuhukumu mtu kwa chaguo lako.

Ukifanya kazi kwa zaidi ya miaka 15 utalipwa fedha ya Pensheni ya Kila Mwezi kutoka NSSF au PSSSF kwa mujibu wa sheria za nchi mpaka siku ya kifo chako.

Utakula bata maisha yote bila kutokwa jasho. Utapata Malipo ya Pensheni ya kila mwezi kulingana na cheo chako. Utaendelea kulipwa kamamstaafu hadi siku kifo kitakapokuondoa duniani. Utakula bila kwenda kazini tena.

Kila mwezi utaingiziwa pesa benki bila kulazimika kwenda kazini. Utakula fedha bata bila jasho maisha yako yote. Mfano kama utastaafu ukiwa na mshahara wa wastani wa shs 1,300,000 mbali na kulipwa kiiunua mgongo, utalipwa pensheni isiyopungua shs 800,000 kila mwezi hadi siku ya kifo chako.

Mfano mwingine; kama utafanya kazi kwa miaka 35 au zaidi na ukastaafu ukiwa na umri wa miaka 60 ukiwa na mshahara wa wastani wa shilingi 3,000,000 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii utakulipa siyo chini ya shs 2,000,000 kila mwezi hadi kufa

kwako. Kwa hiyo kama una taaluma yako na una umri mzuri wa kuajiriwa serikalini au kwenye makampuni na sekta binafsi na unawaza kufanya kazi hadi utimize umri wa kustaafu usiache.

Fanya hivyo upate kazi na utakapostaafu utapata fedha bila jasho uzeeni mwako hadi kifo. Mfano, kama utafanya kazi kwa miaka 35 kisha ukastaafu ukiwa na umri wa miaka 60 na ukaishi duniani miaka mingine 35 utalipwa pensheni mpaka kifo kikuondoe duniani. Changamoto ya utaratibu huo ni kwamba huwezi kuurithisha kwa watoto wako. Ukifa tu ndiyo mwisho wa habari.

3. Wekeza Kwenye Miradi ya Kudumu:

Miradi ya kudumu huleta fedha kwa miaka mingi sana. Nyumba za kupangisha ni mojawapo wa miradi ya kudumu. Nyumba za kupangisha zaweza kupatia kipato-lala kitachokusaidia maisha yako yote. Mfano kama unaweza kujenga nyumba 10 za kupangisha kwa shilingi 300,000 kila mwezi kwa kila nyumba ni kwamba kila mwezikodi ya pango la nyumbazako haitapungua shilingi 3,000,000 kwa kila mwezi.

Pesa hiyo utaipata kwa miaka yote ya uhai wako. Watoto wako hadi wajukuu zako watafurahia kipato hicho bila wao kutokwa najasho lolote.

Wazazi wenye busara huwarithisha watoto wao nyumba. Hata maandiko matakatifu yanathibitisha hilo.

Aidha, unaweza kuwekeza kwenye miradi mingine ya kudumu kama vile mashamba ya mazao yadumuyo kama vile miti ya matunda, mashamba ya miti ya mbao, mashamba ya katani, mashamba ya korosho, mashamba ya chikichi au nazi, n.k. yote hiyo itakuletea fedha kwa kipindi kirefu hadi wajukuu. Miradi mingine ya kudumu nimeifafanua kwenye sura ya 9. Soma sura hiyo ujipange zaidi kupata fedha bila jasho uweze kula bata milele.

4. Wekeza Kwenye Taasisi zitoazo gawio la hisa:

Kama ungependa uwe unapata fedha bila jasho, mbinu nyingine ya kufanya ni hii ya kuwekeza fedha zako kwenye taasisi za fedha zinazotoa hisakila mwaka au kila mwezi. Taasisi hizo ni pamoja na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ambayo hupokea fedha za wawekezaji wa ndani wanaotaka kuwekeza kwenye Hatifungani serikali. Aidha, unaweza kuwekeza kwenye makampuni ya biashara benki za Biashara zinazotoa gawio kila mwezi au kila mwaka. Utalipwa gawio kila mwaka.

Ukitaka fedha yako wakupatie kwa mwezi pia mtajadiliana na wahusika nao watakulipa kwa mwezi. Ukiwekeza kwenye taasisi inayotoa gawio la 10% hadi 14% Kwa mwaka utapata pesa nzuri sana. Taasisi inayotoa gawio kubwa ni Benki Kuu ya Tanzania kwenye Hatifungani zake zinazotoka kupitia minada kila mwaka. Kwa maelezo zaidi ya uwekezaji huu, soma sura ya 8 inayoeleza miradi inayoweza kukupatia fedha bila jasho.

5. Tengeneza “YouTube Channel” yako:

Mitandao ya kijamii ilianza miaka ya 2010 na kuendelea sana hadi sasa. Kwenye mitandao hiyo kwa watu wanaojua kuitumia vyema kuna pesa nyingi za kutosha siku hizi. Watu wengi Tanzania hatujabaini hilo. Kwa upande wavijana Tanzania waliogundua hilo wanapata fedha kubwa sana.

Mitandao ya kijamii inayotumiwa sana na wengi ni pamoja na; Instagram, Facebook, Twitter, YouTube, na mingineyo mingi. Mitandao wa kijamii wa “Youtube” unamilikiwa na Kampuni ya biashara iliyopo Marekani iitwayo “Google”. Mitandao huu unafanya kazi ambazo zilikuwa zikifanywa na televisheni za kawaida. Miaka kadhaa ijayo, televisheni za kawaida zitaondoka kabisa sokoni.

Kwa sasa televisheni za Kijamii zimeongezeka sana zinafanya kazi kama ilivyokuwa vituo vya televisheni vya kawaida. Ukiwekeza kwenye mtandao huo wa YOUTUBE kwa kuweka chaneli yako ya mtandaoni (Online TV) ikapendwa sana, ikatazamwa sana, ikawa na washirika wasiopungua 1000 wenye uwezo wa kutazama video na vipindi vyako kwa zaidi ya saa 4000 na kuendelea, kampuni ya Google ya Marekani itanza kukulipa fedhazitokanazo na matangazo wanayopata.

Kama wewe ni mtu unapenda kupiga picha za matukio mbalimbali zenye kuelimisha, kuburudisha, kuchekesha, mahubiri, mafundisho, nk. Utalipwa na kampuni ya Google kulingana na idadi ya washirika (Subscribers) na watu wanaotazama video zako Youtube na Instagram.

Aidha, makampuni makubwa ya ndani ya nchi yanaweza kukulipa pesa nzuri ili watumie chaneli yako au akaunti yako ya Instagram na Twitter kutangaza biashara zao kama utakuwa una washirika (subscribers, followers, na viewers) wanaovutia kibiashara.

Unaweza kulipwa fedha nyingi sana kutoka kampuni ya Google mpaka ukashangaa.

Kwa Tanzania kuna vijana kama akina Diamond Platinumz mwanamziki wa kizazi kipya, mtu kama Millard Ayo, mtu kama Erick Shigongo, n.k hawa watu wanapata vipato endelevu na vikubwa kutokana na channel zao kwenye mitandao ya Youtube, Instagram, facebook, n.k.

Ukimiliki channel yako na ukaweka vitu vyenye mvuto huko unaweza kulipwa fedha bila jasho kwa miaka mingi kwa kazi uliyoifanya miaka mingi iliyopita. Kama unapenda kupiga picha za video na matukio mbalimbali hiyo ni fursa unayoweza kuifanyia utafiti na uchunguzi zaidi ili uifanye.

6. Andika Vitabu Vya Elimu Mbalimbali

Njia nyingine inayoweza kukupatia kipato kwa miaka mingi ukishamaliza kufanya kazi hiyo ni kuandika vitabu mbalimbali. Andika vitabuna uvichapishe, uvisambaze kila kona ikiwemo mitandaoni (Online publishing). Hakika utapata fedha kwa miaka mingi.

Andika vitabu vya fani mbalimbali kuhusu watoto, ndoa, uchumi, fedha, hadithi, mapenzi, michezo ya mpira wa miguu, kikapu, wavu,

tenisi, siasa, historia, n.k. andika kwa weledi mkubwa.

Sambaza vitabu hivyo kwenye maktaba mbalimbali duniani. Sambaza kupitia mitandao (e-Book publication), sambaza kupitia maduka mbalimbali ya vitabu. Sambaza kupitia njia endelevu hizo utapata fedha endelevu.

Kama unataka hadi watoto wapate fedha za kutokana na kazi zako hakikisha kuwa unawarithisha watoto wako maelezo ambayo yatawasaidia kupata fedha za mauzo ya vitabu au kazi zako hata kama wewe haupo. Mifano ya watu wanaoendelea kupata fedha kutokana na kazi za wazazi wao ipo mingi sana ikiwemo Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere.

7. Tengeneza Filamu au Nyimbo Ruhusu Zirushwe na Runinga (Televisheni).

Kutengeneza filamu zinazopendwa na kucheza kwenye runinga nchini au nje ya nchi ni njia nyingine ya kupata fedha bila jasho kwa miaka mingi.

Kama unacho kipaji cha kutunga filamu, ukazitengeneza vyema kwenye mifumo inayokubalika na vituo vya televisheni, unaweza

kujipatia pesa bila jasho kwa miaka mingi. Tunga filamu na uzitoa kwenye vituo vya Televisheni ndani na nje ya nchi ili ziwe zinachezwa ka mapatano ya kifedha au kibiashara.

Mfano ni filamu za Steven Kanumba aliyefariki akiwa ametoa filamu mbalimbali. Kadri zinavyorushwa kwenye vituo vya televisheni filamu hizo zinaingiza fedha mwaka hadi mwaka.

Mama yake na Steven Kanumba ameendelea kulipwa fedha kutokana na kazi itoshe tu kumalizia hapa kwamba ukitaka kufanikiwa kifedha tengeneza mifumo au miundombinu yenye uwezo wa kutengeneza kipato-lala au “Passive Income” au Kipato Endelevu.

Kila siku unapopata kipato chochote kutokana na ajira yako au kutoka kokote pigania kujenga vyanzo vya mapato vyenye uwezo wa kuleta pesa kwa miaka mingi sana.

Hebu fikiria kuwa na vyanzo vya fedha vitakavyokupatia fedha kwa Miaka mingi sana hata ukiwa umelala au umeondoka duniani. Ni raha iliyoje kula bata duniani bila kuwa na “stress” yoyote ya kuishiwa pesa? Ni raha iliyoje kuwa na vyanzo vya uhakika vya fedha hata ukiondoka duniani?

Naomba kila Mtanzania atakayesoma kitabu hiki ajitahidi kutengeneza vyanzo vya fedha endelevu ili taifa letu liweze kuwa na watu wenye vipato endelevu nje ya ajira au kujiajiri. Tuhimizane kutengeneza mifumo ya biashara amabyo itakuwa na nguvu ya kutiririsha fedha kwa miaka mingi bila kulazimika kumfanya mwanzilishi kufanya kazi.

Wenye hekima wote hufanya hivyo. Wenye Hekima huwaachia watoto wao miundombinu na mifumo ya kuleta fedha hadi kwa watoto wa watoto wao.

Wafanyakazi walioajiriwa na waliojiajiri kila mtu akipambana kutengeneza mifumo, miradi na biashara endelevu kwa nia ya kupata fedha endelevu bila kulazimika kutegemea mishahara au faida za biashara, hapo ndipo taifa letu litakuwa na uhuru wa kifedha.

SURA YA 8

Miradi ya Kuepuka Kufanya Uzeeni

Usifanye Kazi Hadi Uzeeni. Pumzika Ule Bata.

Lengo la sura hii ni kutoa ushauri kwa watumishi walioajiriwa sekta zote ili wanapostaafu wasifanye biashara au miradi kwa kubahatisha au kukurupuka mara tu wanapopata fedha za mafao yao ya uzeeni na pensheni kutoka mifuko ya NSSF au PSSF.

Lengo pia ni kushauri wale ambao wamejajiri na wanadhani wanaweza kufanya miradi mikubwa wakifika umri wa uzeeni.

Mfanyakazi anapostaafu au mtu yeyote akifika umri wa uzeeni siyo kipindi cha kufanya kazi zenye pilikapilika tena kama alivyokuwa akifanya wakati wa umri wa miaka 30 hadi 55. Huo ni umri ambao anatakiwa kula bata tu miaka yake yote iliyobakia.

Ni kweli kwamba mtu anapostaafu anaweza kufanya miradi mbalimbali ya kuweza kumpatia fedha baada ya kustaafuili kumwezesha kufikia ndoto zake kabla ya kuondoka duniani.

Lakini, kutokana na changamoto nyingi za uzeeni na kwenye biashara au miradi mingi, kwa uzoefu na busara zangu; nawashauri wastaafu wasifanyeyafuatayo:

1. Mradi wa Mabasi, Taxi, Bodaboda, Bajaji.

Nawashauri wastaafu wasiwekeze kwenye mradi huu kutokana na kwamba vyombo vya moto huwa havidumu kwa kipindi kirefu.

Mradi wa chombo cha moto kinachohitaji matengenezo makubwa mara nyingi, Kama hujawahi kabisa kufanya mradi huu kabla ya kustaafu, nashauri usijiingize kwenye miradi ya vyombo vya moto. Utachanganyikiwa uzeeni mwako.

2. Mradi wa Kufuga Kuku kwa wingi.

Miradi ya ufugaji kuku kwa wingi (large scale farming) ni miradi ambayo kama hujawahi kuufanya kabla ya kustaafu; nakushauri usiufanye uzeeni.

Endapo zitatokea changamoto za magonjwa navifo vingi vya kuku wako kwa wingi utachanganyikiwa na kufa mapema.

Kama huna uzoefu waufugaji kuku wa kienyeji au wa kisasa kwa angalau miaka 3 au zaidi (kuanzia kuku 100 au zaidi); nashauri usifanye mradi huo uzeeni.

Siyo tu kwamba ni mradi usiodumu kwa miaka mingi lakini pia changamoto zake na pirika zake zitakukatisha tamaa kuendelea na mradi huo kwa maisha yako yote ya uzeeni.

3. Mradi wa Duka la rejareja (Retail Shop):

Ukistaafu nakushauri usifanye biashara ya duka la rejareja mtaani au mjini kama hukuwahi kuwa na duka kama hilo.

Duka la vifaa vya ujenzi, duka la bidhaa mchanganyiko, duka la dawa, duka la nguo, duka la vipodozi, nk.

Kama umekuwa ukifanya biashara hiyo miaka 3 hadi 5 kabla ya kustaafu hapo mimi sina pingamizi sana. Lakini kama unataka mara tu unapostaafu ufanye mradi

wa duka, ukweli ni kwamba siamini kuwa ni biashara itakayokusaidia baada ya kustaafu.

Maduka ya rejareja au madogo madogo waachie watu wenye uzoefu wa maduka au vijana ambao bado wana umri wa kujaribu hiki na kile.

Wewe fanya biashara nyingine endelevu kulingana na umri wako.

4. Mradi wa Kilimo cha Nyanya:

Kama unapanga kulima nyanya baada ya kustaafu, nakuomba uwaze kubadilisha. Kama unapanga kulima mpunga, mahindi, viazi, nk kwa wingi kwa nia ya kutoka kiuchumi baada ya kustaafu; hakika fikiria kubadilisha.

Lakini kama una uzoefu wa zaidi ya miaka 3 katika kilimo cha nyanya haina shida endelea nao huo mradi wa nyanya.

5. Mradi wa Kugombea Udiwani au Ubunge:

Miradi mingine ambayo wastaafu wengi hujiingiza na kuingiza fedha zao za kiinua

Mgongo ni miradi ya kugombea nyadhifa za kisiasa.

Wapo wastaafu wengi huamua kutumia fedha zao zote za kiinua mgongo kwenda kushiriki haki za kikatiba kutafuta kupigiwa kura za uwakilishi wa Udiwani, Ubunge na Urais wakiadini watashinda nyadhifa hizo walizotia nia kugombea.

Tatizo ni kwamba wagombea wengi wanapokosa kuchaguliwa na wananchi huchanganyikiwa na wengine hufariki dunia kwa msongo wa mawazo na *“pressure”*.

Kugombea uongozi wowote wa kutumikia watu siyo vibaya wala siyo dhambi kwa mtumishi aliyestaafu. lakini kama gharama za kampeni zitabebwa na kiinua mgongo chako bila msaada wa chama chako mwanzo hadi mwisho, huenda ukafa mapema kwa shinikizo la moyo.

Epuka kutumia malipo ya kiinua mgongo chako kutafuta uongozi wa kisiasa siyo busara kabisa. Usigombee wadhifa wowote wa kisiasa kwa nia ya kupata pesa kwenye cheo unachokipigania. Uwekezaji huo haufai kabisa kwako.

Nakushauri ukistaafu kazi za ajira usijiingize kwenye siasakwalengo la kupata fedhana marupurupu ya kisiasa. Utachanganyikiwa ukikosa cheo hicho au ukiondolewa kwenye cheo hicho.

Ingia kwenye siasa kwa nia ya kuwatumikia wananchi wa eneo lako siyo kwa nia ya fedha zilizomo katika vyeo vya kisiasa. Ingia kwenye siasa kwa nia ya kuwawakilisha wananchi kwenye vyombo vya maamuzi. Hapo itakuwa sawa.

6. Mradi wa Kukopesha (Microfinance loaning):

Kuna watu wanapostaafu wakilipwa tu fedha za kiinua mgongo huamua kuanzisha miradi ya kukopesha watu kwa riba.

Kama hujawahi kufanya mradi huu wa kukopesha watu wakati ulipokuwa hujastaafu, baada ya kustaafu sikushauri ujiingize kwenye miradi hii ya kukopesha fedha. Utakufa mapema.

Watanzania wengi hawana uaminifu wa kurejesha mikopo. Utamaduni huo huenda

utakuumiza sana na utashindwa kufuatilia marejesho ya fedha zako na hatimaye utakwama na kuchanganyikiwa uzeeni mwako.

7. Usifanye miradi ambayo usimamizi wake Unataka Uwepo Kazini kwa 100% ili ufanikiwe:

Unapostaafu kazi za ajira ninashauri usifanye miradi ambayo itahitaji usimamizi wakokwa asilimia 100.

Mradi wowote au biashara yoyote itakayokuhitaji wewe binafsi uwepo eneo la kazi kusimamia asubuhi hadi jioni, siku saba kwa wiki, miezi 12 kwa mwaka; nakushauri miradi hiyo usiifanye. Miradi au biashara hiyo achana nayo. Utakufa mapema kwa kukimbizana na mradi huo.

Mimi ninavyoona, baada ya kustaafu siyo muda umri mzuri wakufanya miradi au biashara inayokuhitaji kuwepo asubuhi hadi jioni, jumatatu hadi Jumamosi. Januari hadi Desemba. Miradi ya namna hiyo inawafaa vijana au watu ambao bado wana nguvu

nawana miaka mingi ya kufanya kazi hii au ile kila wakati.

Ukistaafu ni wakati wa kuwa na muda mwingi wa kupumzika nyumbani na kula pesa bila jasho. Siyo muda wa kukimbia huku na kule tena. Ni muda wa kufanya miradi ambayo siyo lazima uwepo muda wote eneo la uwekezaji.

8. Ukistaafu Epuka Kuajiriwa tena

Kama ulikuwa umeajiriwa ikifika umri wa kustaafu hakikisha umestaafu kweli kweli. Ukiona mtu anaendelea kufanya kazi za mkataba au kutafuta kazi tena baada ya kustaafu ujue kuwa huyo hajastaafu. Amebadilisha tu aina ya kazi.

Kwa kweli kuendelea kufanya kazi tena za mikataba serikalini au kwenye mashirika au makampuni ni sawa na kusema hujastaafu kazi. Bado uko kazini.

Wapo wastaafu wengi ambao huendelea kuomba kufanya kazi kwa mikataba mwaka baada ya mwaka. Huko siyo kustaafu. Hali hiyo niishara kuwa mstaafu huyo ameamua kuchagua kufanya kazi milele badala ya

kuchagua kula bata miaka yako iliyosalia duniani.

Ndiyo maana hata tajiri mmoja mkubwa sana duniani Bwana **Warren Buffet** anasema kwenye moja ya vitabu vyake hivi:

“Usipotafuta njia za kupata fedha hata ukiwa umelala usingizi, utaendelea kufanya kazi hadi siku ya kifo chako”.

Kabla ya kutimiza umri wa miaka 60; hakikisha kuwa unawekeza kwenye miradi au biashara kubwa itakayokuwezesha kuendelea kupata fedha hata ukiamua kustaafu muda wowote.

Watu wote wenye busara ndivyo walivyofanya tangu zamani za historia. Epuka kufanya kazi asubuhi hadi jioni hadi siku ya kifo chako.

**Think Investment because
you won't be young forever!
Think Entrepreneurship
because you won't be
employed forever!! Be Wise!!!**

Hakikisha unatekeleza miradi na uwekezaji wa vitegauchumi ambavyo vitatengeneza fedha za kutosha matumizi ya kila mwaka kwa miaka mingi sana ijayo.

Kumbuka: Hautakuwa kijana milele kuna siku ajira yako itakoma. Kuna miaka hutaweza kuajiriwa wala kujiajiri tena. Wekeza zaidi na zaidikwenye vitegauchumi vingi uwezavyo.

SURA YA 9

Miradi 15 itakakuyoleta Fedha Bila Jasho

Kuna msemu usemao kwamba asiyefanya kazi asile. Msemu huo kwenye sura hii naomba tuuweke vema kwamba ukiweka miundombinu imara ya kifedha utakula unachotaka maishani mwako hadi wajukuu bila kutokwa jasho.

Ukweli ni kwamba wapo watu wengi sana duniani wanakula fedha nzuri sana bila kwenda kazini kila siku. Walishafanya uwekezaji ambao unawapatia fedha kila wakati bila kulazimika kufanya kazi tena.

Miradi niliyopendekeza katika sura hii, mtu akiifanya na ikaenda vema inaweza kumpatia fedha bila jasho kwa miaka na miaka. Ni miradi ambayo kuitekeleza haihitaji kuisimamia kwa asilimia 100.

Watumishi walioajiriwa nawashauri wasome sura hii na waanze kuitekeleza miradi hiyo ili watakapostaafu kazi za ajira wawe na misingi imara kifedha. Kwa mfanyakazi anayeona mbali sana, miradi hii nitakayoifafanua hapa inawafaa sana.

Mfanyakazi akiwekeza pesa akingali kazini au kabla ya kutimiza umri wa miaka 40 anaweza kuamua kustaafu mapema akiwa bado kijana sana.

Watumishi wanaostaafu na wapo kwenye mchakato wa kulipwa Mafao yao ya Kiinua Mgongo kutoka PSSSF au NSSF hawana budi kujifunza ili waamue kufanya mradi upi baada ya kustaafu. Ukweli ni kwamba hii ni miradi yenye kipatokikubwa na endelevu kuanzia mtu awapo ujanani, uzeeni na hadi wajukuu. Fuatilia mpaka mwisho:

1. Nyumba za Kupangisha katika Miji inayokua haraka nchini
2. Mashamba ya Ufugaji Nyuki (nje ya mji)
3. Ufugaji wa Ng'ombe wa Maziwa (Ng'ombe 4 hadi 8 tu)
4. Hati fungani (Bonds) za Serikali au Mashirika.
5. Mradi wa Kuandika Vitabu Vya Kuuza
6. Mradi wa shamba la Maembe au Parachichi.
7. Mradi wa Shamba la Minazi au chikichi.
8. Mradi wa Shamba la Machungwa au Limao
9. Kuwekeza Katika Akaunti Maalum (Bank Fixed Deposits)
10. Kumiliki Taasisi za Ushauri (Consultants Organisation)

11. Mradi wa Shule ya Awali (Children Daycare Center).
12. Mradi wa Shule ya Msingi na Sekondari.
13. Mradi wa Nyumba ya Kulala Wageni
14. Mradi wa Mashamba ya Miti.
15. Mradi wa Shamba la Miti ya Zabibu.

Naomba nifafanue baadhi ya hiyo miradi 15 niliyoitaja hapo juu.

Sitafafanua kwa mtiririko nilioutaja hapo juu lakini nitakuonesha picha tu ya jinsi unavyoweza kupata fedha bila jasho kwenye miradi hii ambayo watu wengi hawajaijua sana na kuitilia maanani.

Kama miradi hii ingetiliwa maanani, watu wengi wangekuwa matajiri hadi wajukuu zao. Wengi wangepata bata maisha yao yote. Wengi wangepata fedha bila jasho miaka na miaka.

Hebu tazama hapa chini maajabu ya kipato utakachopata maisha yako yote bila jasho:

1. Miradi ya Nyumba za Kupangisha

Una habari kwamba unaweza kuwa na kipato kizuri mwaka hadi mwaka kwa kuwekeza kwenye nyumba za biashara? Fikiria tu kama unaweza kujenga Nyumba 4 kwa shilingi 15,000,000 kila nyumba moja

sawa na shilingi milioni **60** na ukafanikiwa kuzipangisha kwa shilingi 150,000 kila mwisho wa mwezi utapata siyo chini ya shs **600,000**.

Nyumba yenye chumba kimoja, sebule, jiko, choo na chumba kidogo cha chakula au watoto inaweza kukugharimu kuijenga pesa isiyopungua shilingi milioni 15 (15 million shillings worth Small apartments).

Kumbuka kuwa ukianza kupata kipato hicho itakuwa maisha yako yote yaliyosalia. Pesa itaendelea kumiminika miaka na miaka. Uwepo hai au ukiwa haupo duniani hadi wajukuu wako watafurahia uwekezajai wako. Utapata fedha bila jasho maisha yote.

Fikiria kama unaweza kujenga Nyumba 6 kwa milioni 90 hadi 120 na nyumba hizo zikakupatia kati ya shs **1,200,000** hadi shs **1,800,000** kila mwezi maisha yote tena bila jasho!!! Unaonaje ukiwa nanyumba 8 mjini na zote kwa pamoja zikakulipakati ya shilingi **1,600,000** na shs **2,400,000** kila mwezi?

Naamini hadi wajukuu zako hawatakuwa na maisha magumu kwa misingi hiyo utakayowaachia mjini.

2. Mashamba ya Ufugaji Nyuki

Ni mradi ambao hauhitaji muda mwingi sana wa usimamizi. Ni mradi unaoweza kufanywa kwa gharama ndogo sana. Unaweza kuanza kupata fedha hata baada ya muda mfupiwa uwekezaji wako. Kumbuka kuwa asali ina faida nyingi sana kiafya, kifedha na kiuchumi. Waweza kutengeneza shamba lako la kufugia nyuki likawa kama hili:



Hapo juu ni picha ya Mfano wa upangiliaji Mizinga kwenye Shamba la Kisasa la kufugia nyuki.

Shamba la Nyuki laweza Kukuletea Fedha nyingi



Picha ya juu na chini ni mfano wa jinsi unavyoweza kutengeneza mizinga yako ya kufugia nyuki kisasa na ukajipatia kipato endelevu kwa Miaka mingi sana.

Mashamba ya Kisasa ya Nyuki



Hivyo ndivyo unaweza kutengeneza shamba lako la nyuki na kila mwaka ukapata kipato cha bila jashoau *Passive Income*.

Unashauriwa kufuga nyuki mbali na makazi ya watu ili kulinda usalama wa watu. Nyuki wakiwa na asali kwenye mizinga yao wanakuwa wakali. Hivyo wanaweza kushambulia watu.

Tazama Maksio ya Mapato Kwenye Ufugaji Nyuki

Jedwali hili hapa chini linaonesha matarajio (projections) ya mapato yatakayotokana na mizinga kwenye shamba lako kama utalina na kuuza asali mara mbili kwa mwaka.

Mizinga	Lita/Kg	Bei –TZS	Mapato kwa Miezi 6	Mapato kwa Mwaka
20	20	10,000.00	4,000,000.00	8,000,000.00
50	20	10,000.00	10,000,000.00	20,000,000.00
100	20	10,000.00	20,000,000.00	40,000,000.00
200	20	10,000.00	40,000,000.00	80,000,000.00

NB: Kwa mwaka unaweza kupata kipato kisichopungua shilingi milioni themanini kwa kufuga nyuki kwenye mizinga 200 tu.

Kama umevutiwa na mradi huu, wasiliana na Maafisa wa Maliasili kitengo cha Nyuki wakupatie ushauri wa kitalaam na kisheria ili uanze kufuga na kuuza asali ndani au nje ya nchi.

Usisahau kuwatembelea wengine waliofuga nyuki ili ujifunze zaidi na kupata uzoefu kabla ya kuanza kutekeleza mradi huu.

3. Ufugaji wa Ng'ombe wa Maziwa

Mradi wa kufuga ng'ombe wa maziwa umefanyiwa utafiti na watu wengi na imebainika kwamba ni miongoni mwa miradi ambayo haina changamoto (risks) nyingi zinazoweza kukatisha tamaa ya kuufanya mradi huu hata kama huna uzoefu sana wa kufuga. Pamoja na kwamba ng'ombe wa kisasa wa maziwa anapaswa kufugwa kwa uangalifu sana, bado nimradi unaotekelezeka na hauhitaji muda mwingi sana wa kusimamia. Ni vyema kuwa na kijana wa kukusaidia kulisha vyakula. Aidha, ni vyema uwe na Daktari wa Mifugo atakayekupatia ushauri wa kitabibu. Ukifanya hivyo, ng'ombe wako watadumu na watakuingizia maziwa mengi na fedha nyingi kwa kipindi kirefu.

3. Mradi wa Kufuga Ng'ombe wa Kisasa wa Maziwa



Ng'ombe	Lita @ Ng'ombe	Bei @ Lita	Mapato@Siku	Mapato@Mwezi	Mapato kwa Mwaka
2	8	2000	16,000.00	480,000.00	5,760,000.00
4	16	2000	32,000.00	960,000.00	11,520,000.00
6	24	2000	48,000.00	1,440,000.00	17,280,000.00
8	32	2000	64,000.00	1,920,000.00	23,040,000.00

Hebu fikiria kama ukiwa na ng'ombe 2 tu wenye uwezo wa kutoa lita 8 tu kwa siku. Kama kila lita ukiuza kwa shs 2000 ambayo ni bei ya mjini katika miji mingi ya Tanzania, unaweza kuwa na kipato cha zaidi ya shilingi **480,000** kwa mwezi takribani shilingi **5,700,000** kwa mwaka.

Fikiria ukiwa na ng'ombe 6 mjini wenye uwezo wa kutoa lita 24 kwa siku na ukauza lita shs 2000. Kwa siku utakuwa na kipato ghafi kisichopungua shs **48,000** au zaidi ya shs **17,280,000** kwa mwaka. Kama una eneo la kufugia ng'ombe chukua hatua haraka uanze mradi huu. Unalipa sana.

4. Hati Fungani (Bonds) za Serikali

Eneo lingine ambalo wastaafu na watanzania wengi hawajaweka macho yao sana ni kuwekeza pesa zao kwenye hatifungani za za serikali kupitia Benki Kuu (Treasury Bonds).

Ukiwekeza fedha zako Kwenye Hatifungani una uhakika wa kupata kipato cha kutosha kila mwaka tena bila jasho kabisa.

Hatifungani ni nini?

Hii ni hati ya mkataba wa kifedha unayopewa na serikali baada ya kuipa kushinda mnada wa kuipa pesa zako serikali. Hatifungani hutolewa kupitia minada tu ya serikali kwa usimamizi wa Benki Kuu.

Hatifungani hutolewa pale tu serikali inapohitaji kupunguza wingi wa fedha zilizoko mikononi mwa wananchi kwakutangaza zabuni kwa wananchi kwa kuwaomba walete fedha zao kuziwekeza kwenye miradi ya serikali. Serikali inapokea fedha hizo kupitia Benki Kuu na serikali hutumia fedha hizo kutekeleza miradi yake na baada ya kipindi fulani serikali huzilipa fedha hizo kwa wananchi kwa kuwaongezea faida juu yake.

Aina za Hatifungani:

Kuna Hatifungani 6 za ambazo hutofautishwa kwa muda na riba inayolipwa kwa mwekezaji. Hatifungani hizo ni hizi hapa:

- a) Hatifungani ya miaka 2. Faida ni **7.82%** kwa mwaka.
- b) Hatifungani ya miaka 5. Faida ni **9.18%** kwa mwaka.

- c) Hatifungani ya miaka 7. Faida ni**10.08%** kwa mwaka.
- d) Hatifungani ya miaka 10. Faida ni**11.44%** kwa mwaka.
- e) Hatifungani ya miaka 15. Faida ni**13.5%** kwa mwaka.
- f) Hatifungani ya miaka 20. Faida ni**14.49%** kwa mwaka.

Kuna hatifungani za miaka 2 hadi miaka 20. Hatifungani za miaka 3 hadi 20 faida utakayolipwa na Benki Kuu haitatozwa kodi. kukupatia hati hizo ambazo zinakuwa Hatifungani zenye faida nzuri ni za miaka 20 ambazo BoT wanalipa faida ya 14.49% kwa mwaka.

Bank of Tanzania

Publications

Financial Markets

Banking Operations

Banking Supervision

Financial Markets

Treasury Bonds Auction Summary

Auction Summary	
15.49% Treasury Bond 20 Issue No. 6 Auction No. 1 Held On 31/Jul/2019	
1 Redemption Date	1/Aug/2039
2 No. of Bids Received	319
3 No. of Successful Bids	258
4 Highest Bid /100	92.9800
5 Lowest Bid /100	77.9300
6 Minimum Successful Price/100	87.5473
7 Weighted Average Price for Successful Bids	89.2676
8 Weighted Average Yield to Maturity	17.4209
9 Weighted Average Coupon Yield	17.3523
10 Amount Offered Tshs (000,000)	116,600.00
11 Amount Tendered Tshs (000,000)	180,444.20
12 Undersubscribed (+) / Oversubscribed (-) Tshs (000,000)	-63,844.20
13 Successful Amount Tshs (000,000)	141,450.10

Kwenye jedwali hilo hapo juu inaonesha kuwa walioomba kuwekeza kwenye Hatifungani za miaka 20 mwezi Julai 2019 walikuwa watu 319 na kati yao waliofanikiwa kupatiwa fursa ya kuwekeza Julai 2019 walikuwa 258 (No. of Bids received 319 and number of successful Bids 258).

Ukisoma kwenye jedwali hilo namba 4 na 5 zinaonesha kuwa walioomba kwa bei ya juu

kabisa waliomba kwa bei ya shilingi 92.9800 kwa kila shilingi 100 na bei ya chini ilikuwa 77.9300.

Wawekezaji walioomba wawekeze kwa bei ya chini (minimum successful price/100 walifanikiwa kwa bei ya shs 87.5473 kwa kila shs 100 iliyowekezwa. Kwa wastani bei iliyochukuliwa na Benki Kuu kwa wawekezaji wote ilikuwa shs 89.2676 kwa kila shs 100 iliyowekezwa na wawekezaji hao.

Kwenye jedwali hilo pia, utajifunza kuwa serikali ilikuwa inahitaji wawekezaji watoe fedha zipatazao shilingi bilioni 116.60 lakini wawekezaji waliojitokeza walikuja ja jumla ya bilioni 180.444 (Tazama namba 10 na 11 kwenye jedwali).

Jambo la kufurahisha ni kwamba wawekezaji wote waliofanikiwa kuwekeza walipewa mkataba wa 17.42% badala ya 14.49% ambayo ndiyo riba ya kawaida kwa mkataba wa miaka 20. Kwa hiyo waliowekeza Julai 2019 watalipwa 17.42% kwa mwaka hadi tarehe 01 Agosti 2039 siku ya kuiva kwa mkataba (Weighted average Yield to Maturity). Tazama Namba 1, 8 na 9 kwenye jedwali hapo juu.

Faida za Hatifungani:

Kama nilivyoeleza kwenye mifano ya miradi na biashara nyingine hapo juu, lengo langu ni kuwaonesha watazania fursa zilizopo nchini zenye uwezo wa kutoa kipato bila jasho kwa mwekezaji.

Faida ya kwanza: Haijalishi ni kijana, mtu mzima au mzee mstaafu, nk. Ukiwekeza kwenye hatifungani hautapata hasara hata kidogo. Hatifungani ni uwekezaji ambao hauna hasara wala hatari za kupoteza mtaji wako wala faida yako (risk free investment).

1.0 Notice

- This new prospectus only applies to bonds issued under the new terms and conditions. Already issued bonds will continue to be governed by the original prospectus and will continue to be traded over the counter.

1.1 Advantages of Treasury Bonds

- They are transferable and negotiable.
- They can be pledged as collateral.
- The rate of return is competitive.
- They are issued through market-based procedures.

Faida ya pili: Ukiwekeza katika Hatifungani una uhakika kwamba serikali haiwezi kukudhulumu haki yako hata kidogo. Hata kama Viongozi wa serikali watabadilishwa, mikataba yako itaendelea

kuheshimiwa na kutekelezwa (Tazama jedwali hilo hapo juu kwenye “1.0 Notice”).

Faida ya tatu: Hatifungani inaweza kurithishwa kwa watoto wako au mtu yeyote. Kama umeingia mkataba na serikali kwenye Hatifungani ya miaka 20 na unadhani hutaweza kuishi kwa miaka yote hiyo, unaweza kuiweka kwenye WOSIA wako ili kama ukifariki dunia ni nani ungependa aendelee kupokea fedha zako za faida na baadaye mtaji wako (T/Bonds are transferable).

Faida ya nne: Hatifungani zinaweza kutumika kama DHAMANA kwenye kuchukua mikopo popote pale kwenye taasisi za fedha na mashirika mengine (T/Bonds can be pledged as collateral).

Faida ya tano: Hatifungani huwa hazitolewi kwa ujanja ujanja wowote. Hatifungani hutolewa kwa utaratibu wa kisheria na hakuna ulaghai wowote unaoweza kufanyika. Siku hizi wameboresha zaidi wanatumia mfumo wa mtandaoni na hauna sababu ya kwenda kuonana na mtu yeyote (They are issued through markets procedures).

Faida ya Sita: Hatifungani hukupa faida yako kila baada ya miezi 6 bila usumbufu wowote kupitia akaunti yako ya benki kwa mfululizo wa miaka

yote uliyowekeza na wakati huo huo mtaji wako upo pale pale hadi siku ya mwisho. Kipindi cha uwekezaji wako kikifika ukomo (yield maturity or redemption date) utalipwa mtaji wako wote bila kujalisha kuwa ulishalipwa faida kwa kipindi chote cha uwekezaji wako.

Maksio ya Kipato unachowezakupataukiwekeza Kwenye Hatifungani za Serikali:

Hebu ona mifano ya jinsi unavyoweza kutengeneza fedha bila jasho kila mwezi kila mwakakwa mfululizo wa miaka 20 ijayo:

Mfano wa kwanza; ukiamua kuwekeza Shs **50,000,000** kwenye hatifungani ya miaka 20 ambayo huwa inatolewa kwa faida ya **14.49%** kila mwaka utapata faida ipatayo shs **603,750.00**. Faida hiyo utaipata kila mwezi bila jasho kwakwa zaidi ya miaka 20 mfululizo hadi mkataba wako utakapofikia ukomo.

Faida hiyo kwa mwezi ukiiweka kwa mwaka ni sawa na **Shs 7,245,000**. Faida hii ni kubwa sana. Inamzidi mtu aliyewekeza kwenye majengo ya kupangisha. Badala ya kujenga nyumba yenye thamani ya milioni 50 itakayokuingizia shs 3,600,000 kwa mwaka ni afadhali ukawekeza

kwenye Hatifungani ambayo itakuingizia zaidi ya ya shs 7,245,000 kwa mwaka.

Mfano wa pili; Ukiwekeza shilingi 100,000,000 (milioni mia moja) kwa faida ya 14.49% kwa mwaka; unapata **Shs 1,207,500.00** kwa mwezi. Faida hii ni sawa na shilingi **14,490,000.00** kwa mwaka. Na kwa kipindi chote cha miaka 20 utaendelea kulipwa pesa hiyo bila tatizo lolote na bila jasho lolote kwa mfululizo wa miaka 20 na mtaji wako ukiwa pale pale. Miaka 20 ikiisha utarudishiwa pesa yako yote uliyowekeza bila kujali faida uliyokwishalipwa.

Benki Kuu ya Tanzania ndiyo itakuwa inakulipa kupitia akaunti yako ya benki yoyote uliyochagua. Faida hiyo ukijaribu kuilinganisha na uwekezaji mwingine, utaona kuwa kuwekeza kwenye Hatifungani kuna faida kubwa zaidi ya kuwekeza kwenye jengo la kupangisha lenye thamani ya shilingi milioni mia moja.

Jedwali la Kipato utakachopata Ukiwekeza Kwenye Hati fungani.

Huu nimfanowa kipato unachoweza kupata kwa miaka 20 kama utawekeza kwenye Hati fungani za miaka 20za Benki Kuu:

Maksio ya Kipato Utakachopata Ukiwekeza Kwenye Hatifungani ya Miaka 20				
AINA YA HATIFUNGANI	MTAJI WA KUWEKEZA	RIBA YA FAIDA	MAKSIO YA FAIDA KWA MWEZI	MAKSIO YA FAIDA KWA MWAKA
MIAKA 20	10,000,000.00	14.49%	120,750.00	1,449,000.00
MIAKA 20	20,000,000.00	14.49%	241,500.00	2,898,000.00
MIAKA 20	40,000,000.00	14.49%	483,000.00	5,796,000.00
MIAKA 20	60,000,000.00	14.49%	724,500.00	8,694,000.00
MIAKA 20	80,000,000.00	14.49%	966,000.00	11,592,000.00
MIAKA 20	100,000,000.00	14.49%	1,207,500.00	14,490,000.00
MIAKA 20	150,000,000.00	14.49%	1,811,250.00	21,735,000.00
MIAKA 20	200,000,000.00	14.49%	2,415,000.00	28,980,000.00
MIAKA 20	300,000,000.00	14.49%	3,622,500.00	43,470,000.00
MIAKA 20	500,000,000.00	14.49%	6,037,500.00	72,450,000.00

Chanzo: Uchambuzi binafsi sera za Benki Kuu ya Tanzania kuhusu Hatifungani za Serikali mwaka 2019.

NB: Kumbuka kuwa uwekezaji wa kwenye Hatifungani ndiyo uwekezaji salama sana duniani (Most risk free investments). Faida yako na mtaji wako vitalindwa na sheria za Benki Kuu kwa miaka yote. Usalama wa mtaji wako na faida ni asilimia 100.

Jinsi ya Kuwekeza Kwenye Hatifungani za Serikali

Hatua ya kwanza ni kujifunza somo hili na kuvutiwa nalo kwanza. Ni vyema kuvutiwa kwanza na uwekezaji huu kabla ya kuchukua hatua yoyote.

Hatua ya pili: Tembelea Mabenki ya Biashara hasa benki ya NMB, CRDB na mengine kama hayo. Benki zote za Biashara ni mawakala wa Benki Kuu ya Tanzania. Wanajua Hatifungani za Serikali.

Ukifika kwenye Kaunta za Mabenki ya Biashara waambie kwamba unataka kufungua akaunti za kuwekeza na Serikali kwenye Hatifungani au kwa kifupi ni CDS yaani “Central Depository System”. Watu wa mabenki ukiwaambia hivyo wataelewa unachotaka. Utapewa Fomu za kujaza. Ukikamilisha ufunguaji wa akaunti hiyo ya CDS fedha unazotaka kuwekeza zitawekwa humo na zitasubiria Benki Kuu ikamishe mchakato wake.

Mchakato wa Benki kuu ukifikia hitimisho na wewe ukawa umechaguliwa au ombi lako limepitishwa (umeshinda mnada) fedha zako zitachukuliwa kutoka kwenye akaunti yako kwenda Benki Kuu. Hapo utakuwa umekamilisha mchakato wa kuwekeza kwenye hatifungani.

Kwa msaada zaidi usisite kuwasiliana na wataalam wa Benki zote za Biashara wanaohusika na kitengo hicho ili wakupe ushauri na maelekezo zaidi au tembelea tovuti ya Benk Kuu.

Changamoto ya Hatifungani za Serikali:

Changamoto ya kwanza: zilizopo kwenye kuwekeza katika Hatifungani ni kwamba uwekezaji wake huwa unatakiwa kuwa na mtaji mikubwa kuanzia shs 5,000,000 kwenda juu kulingana na ukomo wa mtaji wako. Kama una mtaji chini ya huo siyo rahisi kupata nafasi ya kuwekeza kwenye Hatifungani za serikali.

Changamoto ya pili: Kuwekeza kwenye hatifungani huruhusiwi kutoa pesa yako kabla ya muda wa mkataba wako kuisha. Kama ni mkataba wa miaka 3, miaka 10, miaka 15, na miaka 20 lazima usubiri kipindi hicho kifike mwisho ndipo utaweza kulipwa pesa yako yote uliyowekeza (You will be paid back your invested capital at maturity age not otherwise).

Changamoto ya tatu: Hatifungani zote lazima zitolewe kwa MINADA ya masoko ya fedha. Unaweza kuomba kuwekeza na ukakubaliwa au ukakataliwa. Kuna kushinda mnada au ukakosa.

Minada ya fedha wakati mwingine inahitaji uwe na uelewa mpana sana ili kuweza kujua mbinu mbalimbali za kushinda minada hiyo.

Waweza Kuwekeza Pia Kwenye U.T.T AMIS

Hatifungani za U.T.T AMIS (Unit Trust of Tanzania Asset Management and Investors Services) nazo ni chanzo cha mapato ambazo nakushauri pia uzitazame na uwekeze pesa yako. U.T.T ni Mifuko iliyopo chini ya Wizara ya Fedha Tanzania. Ni Mifuko salama kuwekeza mtaji wako kwa sababu inaangliwa na Serikali. Mifuko ya U.T.T ipo 6 na inatoa gawio kila mwezi, kila baada ya miezi sita au kila mwaka kulingana ukubwa wa mtaji wako.

Uzuri wa Mifuko ya UTT ni kwamba ni rahisi kuwekeza na haina taratibu ndefu sana kuwekeza mtaji wako. Unaweza hata kutumia simu yako kuwekeza kuanzia shs 50,000 na kuendelea tofauti na Benki Kuu ambapo mtaji wake lazima uwe mkubwa. Kwenye UTT watu wanaopenda kuwekeza wanaruhusiwa kuwekeza bila kutumia utaratibu wa minada (Auctions) kama inayotumiwa na Benki Kuu.

Utaratibu wa kuwekeza kupitia U.T.T (Unit Trust of Tanzania) unaweza kuupata katika ofisi za Shirika la Posta au unaweza kwenda Benki ya

CRDB ambayo ipo kila mkoa utapewa maelezo ya kutosha kuhusu uwekezaji kwenye UTT. Aidha, waweza kupata maelezo yao kwenye mtandao wao kupitia tovuti hii hapa, “<https://www.uttamis.co.tz>” .

Kumbuka: Faida au riba itolewayo na U.T.T iko chini ya ile itolewayo na Benki Kuu kwa sababu wao pia wanawekeza kwenye hati fungani za Benki Kuu.

5. Mradi wa Kuandika Vitabu

Unaweza kuwa mwandishi wa vitabu ukawa unaviuza kwa wadau wako na ukapata pesa ya kukutosha kwenye maisha yako. Kama unao uzoefu wowote kwenye maisha haya unaweza kuutumia uzoefu huo kama fursa ya kipato kwa kuandika vitabu na kuvisambaza viuzwe.

Kuandika Vitabu Mbalimbali

- Mradi mwingine unaoweza kukupatia fedha ni kuandika vitabu mbalimbali vya; Uzoefu wako, Elimu ya kitaaluma, Maarifa yako, au vya Hamasa za maendeleo(Motivational Books).


Mfano:

Ukitoa **Vitabu nakala 3000** Ukapata faida ya Shs 2000 @ kitabu utapata zaidi ya **shs 6,000,000**


Je, Vitabu elfu 10?

Faida shs 20,000,000??

Hata mimi nimekuwa nikiandika vitabu mbalimbali. Naandika vitabu kama mradi wangu lakini pia kama kitu ninachokipenda. Napenda kuandika sana. Napenda kusoma pia kazi za watu wengine. Mradi wa kuandika vitabu ukiufanya kama kazi yako unayotaka ikulipe kipato hakika utapata malipo siyo haba. Tazama picha za mifano ya vitabu nivyowahi kuandika kuanzia mwaka 2014. Hadi sasa nimeshaweza kuandika vitabu 7 na hiki ulichonacho ni cha 8.



Kitabu Changu cha mwaka 2018



Hiyo ni mifano ya Vitabu vyangu zaidi ya Saba ambavyo nimewahi kuchapisha tangu mwaka 2014 nilipoanza kazi za uandishi.

6. Mradi washamba la Maembe au Parachichi.

Unapoajiriwa tu kazi yoyote nakushauri mshahara wako ikiwezekana asilimia hamsini (50%) uelekeze kwenye kulima shamba la matunda aina ya embe. Ni vema ukajitahidi kupata shamba la ukubwa wa Hekari 1, hekari 2, hekari 4, hekari 6 au hekari 10 au zaidi kulingana na ndoto yako unayoitaka.

Miti ya maembe inaweza kudumu kwazaidi ya miaka 40 huku ukiwa unavuna matunda yake na kupata fedha zitokanazo na matunda hayo bila jasho kabisa. Utafanya kazi ya kulitunza shamba lako kwamiaka 3 au 5 ya mwanzoni tu. Baada ya hapo ni mwendo wa kula maembe na maparachichi huku ukila pesa yake bila jasho tena. Wanunuzi watakuletea fedha ulipo.

Miradi ya mashamba ya Matunda



Miradi hiyo ya mashamba ya matunda inafaa sana ukiianza miaka 3 au 5 kabla hujaamua kustaafu kazi za ajira. Kutegemeana na aina za mbegu utakazoamua kupanda. Lakini ushauri wangu ni kwamba ni vyema kupanda mbegu za matunda yanayokomaa kuanzia miaka 3 au 5 ili

mwaka ule utakaostaafu miti hiyo iwe tayari imekomaa na inatoa matunda yawezayo kuuzika sokoni.

Tazama faida au kipato unachoweza kupata kama utakuwa na shamba la miembe lenye uwezo wa kuzalisha maembe 200 tu kwa kila mwembe mmoja kwa mwaka:

IDADI YA MIEMBE SHAMBA NI	IDADI YA MAEMBE UTAKAY OUZA @ MWAKA MITI YOTE	BEI YA EMBE MOJA	MAKSIO YA PATO KUU KWA MWEZI	MAKSIO YA PATO KUU KWA MWAKA
MIEMBE 100	20000	300	500,000.00	6,000,000.00
MIEMBE 300	60000	300	1,500,000.00	18,000,000.00
MIEMBE 500	100000	300	2,500,000.00	30,000,000.00
MIEMBE 700	140000	300	3,500,000.00	42,000,000.00
MIEMBE 1000	200000	300	5,000,000.00	60,000,000.00
MIEMBE 2000	400000	300	10,000,000.00	120,000,000.00

NB: Maksio haya yamechukuliwa kwa kuamini kwamba mti mmoja wa mwembe waweza kuzalisha maembe 200 kwa mwaka hasa kwa Mwembe uliokomaa kuanzia umri wa miaka mitano. Hekari moja lenye ukubwa wa 70 x 70

linaweza kupandwa miti ya miembe ipatayo 60 hadi 100.

Kwa hiyokama ukiwa na hekari moja lenye miembe 100 na kila Mwembe ukazalisha matunda yapatayo 200 na kila embe ukaliuza kwa bei ya shambani shs 300 unaweza kujikuta kwa mwaka unapata kipato kisichopungua $\text{shs } 300 \times 200 \times 100 = \text{shs } 6,000,000$. Kumbuka: haya ni maksio tu siyo lazima iwe hivyo hivyo. Lakini inakupatia sura inayofanana.

Ukitaka Mafanikio uwe tayari Kuchekwa na kuchorwa



Pinda anatafuta utajiri kwa kuuza embe

Ukiwa na hekari 3 zenye Miti ya miembe ipatayo 300 unaweza kupata kipato cha zaidi ya shs 18,000,000 kwa Mwaka.

Ukiwa na hekari 5 zenye miembe ipatayo 500 baada ya miaka 5 ya kuvumilia unaweza kuanza kujipatia kipato kisichopungua shs 30,000,000 kwa mwaka.

Ukiweza kuwa na hekari 10 za miti ya miembe 1000 kwa mantiki hiyo hiyo unaweza kujipatia kipato kisichopungua shs 60,000,000 kwa mwaka. Hii ni sawa na shs 5,000,000 kwa mwezi.

Ukiamua moyoni mwako kufanya mradi huu ukingali kazini au ukiwa bado na umri wa ujana au ukiwa umebakiza miezi 60 kustaafu, unatafanikiwa. Hata kama ni Miparachichi, mananasi na matunda mengineyo. Chukua hatua leo usiaibike uzeeni.

7. Mradi wa Mashamba ya Miti ya Mbao.

Kama unavyoweza kuona kwenye picha ya shamba langu binafsi la miti hapo chini nililolipanda mwaka 2015 mwanzoni. Wewe pia unaweza kuamua kuwekeza kwenye mashamba

ya miti ya mbaona baadaye itakulipa fedha bila jasho.

Hebu fikiria kama una miti 2000 na kila mti ukakupatia mbao za thamani ya shs 300,000 na ukauza miti yote 2000 baada ya miaka 15 tufanye hata kama ni baada ya miaka 20. Utapata kiasi gani cha pesa? Ukiuza miti hiyo 2000 kwa shs 300,000 kila mti utapata fedha siyo chini ya shs 600,000,000.



Picha hii ni shamba langu binafsi la miti lililopo Kigoma. Miti hiyo ilipandwa Januari 2015. Miti hiyo inatarajiwa kukomaa kuanzia mwaka 2025.

Baada ya miaka 20 tu unapata shilingi milioni mia sita!!! Hakuna mfanyakazi wawa kuajiriwa anayepata pesa hiyo akistaafu baada ya kufanya kazi miaka 20. Je kama una miti 4000 tu? Je kama una miti zaidi ya elfu 20 itakuwaje? Piga hesabu. Chukua hatua leo leo.

8. Mradi wa Shamba la Zabibu

Taifa la Israeli ni maarufu kwa kilimo cha Zabibu tangu zamani za kale. Zabibu ilitumika kwenye matukio mengi ya kifalme (Royal events) na hadi leo hii vinywaji vitokanavyo na zabibu vinaheshimika kote ulimwenguni. Kwa hiyo zabibu ni zao lenye soko kote duniani.

Kama ungependa kupata fedha bila jasho kwa miaka mingi, Unaweza kuwekeza kwenye mashamba ya zabibu kama mzee Peter Mizengo Pinda (Waziri Mkuu Mstaafu) anavyofanya katika kijiji cha Zuzu nje kidogo ya Jiji la Dodoma. Ukweli ni kwamba hiki ni kilimo ambacho kitakupatia kipato kwa kipindi kirefu sana. Mradi ukiishakamilika utavuna mazao yake na kuyauza kwa kipindi kirefu. Utavuna pesa kwa miaka na miaka.

Watu wengi wanatumia zabibu sana Tanzania na nje ya Tanzania. Hivyo, soko la zabibu ni kubwa

sana. Fanya utafiti wa kutosha ni mkoa gani uwekeze kwenye Zabibu maana siyo mikoa yote zabibu inastawi. Kama uko mkoa wa Dodoma na mikoa mingine ambayo zabibu hustawi usiache kuwekeza kwenye mashamba ya zabibu kama unavyo kwenye picha ya Mzee Pinda hapa chini.



Shamba la Mzibabi kwa Mizengo Pinda, nje ya Jiji la Dodoma.

Shambani kwa Kayanza Peter Pinda



Ukitembelea shamba la Mheshimiwa Mzee Kayanza Pete Pinda Jijini Dodoma hautakosa somo unalotoka nalo kwenda kulifanyia kazi.

9. Mradi wa Nyumba za Wageni (Guest Houses)

Pamoja na kwamba miradi ya nyumba za kulaza wageni mijini zinahitaji fedha nyingi sana; mtu anayetaka miaka mingi ijayo apate fedha bila kutokwa jasho, anaamua kuwekeza kwenye miradi hii ya nyumba za kulaza wageni mijini.

Anaanza mapema tu akiwa bado ana umri wa kawaida tu hata kuanzia umri wa miaka 30 ili mradi uwe na nia na mradi huo. Nina imani mtu huyo akitimiza miaka 55 ataanza kula fedha bila jasho hadi uzeeni na mpaka wajukuu wake watanufaika na mradi huu wakiuendeleza vema.

Ukipenda mradi huu wa nyumba za wageni, unaweza kuamua kuanza na nyumba moja tu hata kama ni ya vyumba 4 tu vya kuanzia kulaza wageni kwenye mji mmoja.

Tufanye mfano, kama Nyumba hiyo italaza wageni wanne kila siku kwa bei ya shs 10,000.00 kwa kila siku kwa kila chumba utaona kwamba kwa mwezi hautakosa kipato cha wastani wa shilingi 1,200,000 mapato ghafi kabla ya matumizi.

Nina imani nyumba hiyo kama ipo maeneo yenye mzunguko wa watu wengi inaweza kukuwezesha kujenga nyumba nyingine zaidi na zaidi na ukapata faida sana. Siyo lazima nyumba ya kulala wageni iwe ya vyumba vingi sana. Hata kama ni vyumba 2, 4 au 6 wewe jenga nyumba hiyo tu. Anza na kidogo kidogo tu. Anzia hali ya chini kwenda juu. Siku moja utanikumbuka sana.

Hebu fikiria kama ukiweza kujenga nyumba ya wageni (Guest House and Hotel) yenye Vyumba 15 na kila chumba kikawa kinauzwa kwa bei ya shs 40,000 kwa siku? Je, unajua kuwaunaweza kupata kipato kisichopungua Shs **600,000** kwa siku kama mapato ghafi?

Je, wajua kwamba kwa mwezi unaweza kuingiza pato la zaidi ya shs **18,000,000**? Je wajua **kwamba** kwa mwaka shs **216,000,000** zitaanza kutoka mapato ghafi kwa miaka na miaka.

Fikiria ukiweza kujenga nyumba ya kulaza wageni yenye Vyumba 20 kwa bei ya shs 25,000 tu kwa siku unaweza kujipatia kipato kisichopungua Shs 500,000 kama mapato ghafi. Ambapo kwa mwezi unaweza kuingiza pato la zaidi ya shs 15,000,000 (milioni kumi na tano kwa mwezi).

Kwa mwaka ni sawa na kipato cha zaidi ya shilingi milioni mia moja na themanini (180,000,000).

Miradi ya nyumba za kulaza wageni kwenye miji inayokua kwa haraka inaweza kukutoa kimaisha mpaka wajukuu zako wote kama utaisimimamia vyema.

Anza mradi huu ukiwa bado na umri wa miaka kati ya 30 na 50 ili utimizapo umri wa miaka 55 au 60 uwe tayari unapata kipato. Epuka kukurupukia miradi ambayo hujafanya utafiti na upelelezi wa faida na hasara. Hata baada ya kujisomea kitabu hiki hakikisha kuwa unafanya upekuzi wa habari na taarifa kwa kila mradi kabla hujaanza kuutekeleza.

10. Mradi wa Shuleya Msingi au Sekondari

Miradi mingine ambayo inaweza kukupatia fedha ukiwa hutoki jasho kwa miaka mingi ni miradi ya shule za binafsi zinazoendeshwa kibiashara. Wapo watu wengi sana waliofanikiwa kwenye miradi hii.

Unaweza kuanza na Shule ya Awali. Ukajenga madarasa 2 au 4 au 7 kulingana na uwezo wako. Lakini siyo lazima kuanza na madarasa mengi. Jambo kubwa ni ndoto uliyo nayo. Kama umesomea ualimu na unao uzoefu wa kufundisha unaweza kuanzisha shule yenye wanafunzi wachache. Hata kama ni wanafunzi 10 au 30 wewe anza tu. Usitake kuanzia juu sana. Anzia mahali ili uweze kufikia ndoto yako ya kumiliki shule kubwa.

Aidha, unaweza kuanzisha Chuo cha Ufundina ukadahili wanafunzi. Chuo cha ufundi wowote. Hata kama ni ufundi wa kushona, uashi, useremala, nk. Unaweza kuwekeza kwenye shule ya Sekondari aushule ya msingi na ukapata fedha kutoka kwenye ada za shule. Wawekezaji wote waliowekeza kwenye miradi hiyo wameweza kupata kipato kwa miaka mingi sana.

Pamoja na kwamba miradi hii huhitaji fedha nyingi bado ukiamua unaweza kuanza tu mapema kabla ya kustaafu kwa kuanza na hatua za chini ili uweze kwenda juu mwaka hadi mwaka.

SUCCESS

WILL NOT COME

TOMORROW

UNLESS

YOU START

TODAY

**MAFANIKIO HAYATAKUJA KWAKO KESHO
USIPOANZA KUYATAFUTA LEO**

SURA YA 10

Kwa nini Watu Hustaaifu Kazi

Sababu za Kustaafu Uzeeni Badala ya Ujanani.

Mazingira ya wafanyakazi wa Tanzania hubadilika kulingana na utawala uliopo madarakani kisiasa. Kwa mfano sababu nyingi za mtu kuamua kustaafu kazi za kuajiriwakwa awamu ya Tano nyingi zaweza kuwa tofauti na zile za awamu ya nne, ya tatu au hata ya kwanza.

Kwa uchache zifuatazo ni sababu kadhaa huwasukuma watu kustaafu hasa Tanzania:

1. Kutimiza umri wa miaka 60. Kwa mujibu wa sheria za Tanzania mfanyakazi akitimiza umri wa miaka 60 **lazima** aondoke kazini kwa kustaafu kwa lazima.
2. Kutimiza umri wakustaafu kwa hiari kuanzia miaka 55 hadi 59. Mfanyakazi wa Tanzania anaweza kuamua kustaafu kwa hiari muda wowote katika umri huo na akalipwa mafao yake kutoka kwenye

Mifuko ya hifadhi ya jamii (PSSSF au NSSF).

3. Kuamua kuacha kazi kwa sababu za kisiasa. Wapo wanaostaafu kazi za ajira waende kugombea nyadhifa mbalimbali za kisiasakama vile udiwani na ubunge.

Lakini kuna wengine hasa wenye nyadhifa za kuteuliwa na Mkuu wa nchi, wakitenguliwa nyadhifa zao huamua kustaafu mapema.

4. Kuchoka kazi za kuajiriwa na kutotaka kuajiriwa tena. Wapo watu huamua kustaafu kwa sababu wamechoshwa na karaha za kuajiriwa. Wengi wa kundi hili huona ajira kama haina uhuru. Wanaona ni kama utumwa na huamua kustaafu ili wawe na maisha ya uhuru wanaoutaka nje ya ajira. Mtu anachoshwa na kazi za ajira kiasi kwamba hataki tena kufanya kazi za kuajiriwa. Hapo anaamua kustaafu.

5. Malengo aliojiwekea mtu mwenyewe yakitimia tu anaamua kustaafu kazi za ajira. Kuna watu wanajiwekea malengo ya kutimiza na wakishayatimiza

wanaamua kustaafu kazi za kuajiriwa. Mfano, mtu aliyeweka lengo la kukusanya akiba fulani ya fedha ikitimia fedha hiyo anaweza kuamua kustaafu kazi ili akajijiri.

6. Mazingira ya kazi kutokuwa rafiki na huru tenakwake ama kutokana na sababu za kisiasa au kikazi. Kuna nyakati mazingira ya kazi yanabadilika na kuwa na sintofahamu kati ya mwajiriwa na uongozi kiasi kwamba mtu anaamua kuchukua hatua za kuacha kazi au kustaafu ili aweze kuishi nje ajira hiyo.

Mazingira ya kazi kubana, mikopo mingi isiyolipika, uchumi kubana, uhamisho wakikazi, kushushwa cheo, n.k hayo yote yanaweza kuwa sababu ya mtu kuamua kustaafu kazi za kuajiriwa hata kabla ya kutimiza umri wa miaka 55 au 60.

7. Kutajirika haraka au kufanikiwa haraka nakupata fedha nyingi zaidi ya mshahara na kuamua kustaafu kazi. Watu wanaoanzisha biashara fulani na kufanikiwa sana kifedha huamua kustaafu.

Kundi hili huwa halisubiri umri wauzee wa miaka 55 au 60 ndipo wastaafu. Hata kama ana umri wa miaka 40, 45 au 50 anaweza kustaafu. Hii huitwa kustaafu kijana ukiwa tajiri (Retire young and retire rich).

8. Mabadiliko ya sheria za Mafao ya Uzeeni. Wapo watumishi wengi huamua kustaafu kwa sababu sheria za mafao ya uzeeni zimebadilishwa.

Mabadiliko ya Sheria na kanuni za kukokotoa mafao kutoka mafao makubwa kwenda madogo yaweza kusababisha watu wengi kuamua kustaafu kabla ya wakati waliopanga kustaafu.

Kwenye kipindi cha mabadiliko ya kanuni za mafao watu wengi wanaweza kuamua kustaafu kukwepa kujikuta wakilipwa mafao madogo miaka ijayo.

SURA YA 11

Maana ya Kustaafu

Raha ya Kustaafu na Ukiwa Bado Kijana

Kustaafu kumekuwa kukitazamwa na wengi kama ni jambo linalofanywa na watu walioko kwenye ajira rasmi tu tena waliozeeka. Hakuna watu wenye umri wa miaka 35 wanaoamua kustaafu. Kila anayestaafu ni mzee.

Ukweli ni kwamba kila mtu angependa kustaafu kazi yoyote baada ya kuifanya kwa kipindi kirefu bila kujali umri wake tangu azaliwe. Hebu fikiria mwalimu au Mhasibu aliyefanya kazi hiyo kwa miaka 15 au 20 au 25 lakini umri wake bado ni miaka 35 au 40 au 45 ?? Kwa nini usistaafu hiyo kazi?

Hata kama umejiajiri ni lazima upange kustaafu kazi unazozifanya. Kuna nyakati unapaswa kupumzika. Hebu nikudokezee kwa kifupi maana ya kustaafu:

1. Ni kupumzika kabisa kufanya kazi za kila siku.
2. Ni kustarehe na kula bata, kufurahia kazi ya mikono yako uliyofanya muda mrefu.

3. Ni kuamua kutoa nafasi za ajira kwa kizazi kipyaa. Kizazi kimoja hupisha kingine.
4. Ni kutulia ili kula matunda ya jasho lako.
5. Ni kukaa kivulini kula mavuno uliyovuna kwenye Jua kali (mchumia juani hulua kivulini).
6. Kustaafu ni wakati wa kula Pensheni yako ukiwa umetulia bila jasho lolote.
7. Kustaafu ni kwenda nje ya uwanja wa mchezo ili uwatazame wengine wanavyocheza mchezo huo kwa ubora zaidi.
8. Ni kuamua kuwaachia wengine wamalizie kazi zilizosalia. Huwezi kumaliza kazi zote.
9. Kustaafu nikuacha kazi zote za kutokwa jasho na kuanza kula fedha bila jasho.
10. Kustaafu kazi ni hatua ya kwenda kwenye likizo ndefu isiyokuwa na ukomo.
11. Kustaafu ni kuamua kuwa mshauri badala ya kuwa mtendaji.

NB: Epuka kutafuta ajira za mikataba baada ya kustaafu, Utafanya kazi hadi kufa kwako.

SURA YA 12

Uhuru wa Kifedha ni nini?

Hapa Tanzania somo hili sidhani kama linafundishwa kwenye shule zetu, vyo vyetu, makanisani, misikitini, mitaani, majumbani. Ni somo adimu sana kufundishwa.

Uhuru wa kifedha umetafsiriwa na waandishi wengi sana duniani.

Uhuru wa kisiasa ni mzuri sana. Lakini uhuru wa kifedha ni zaidi.

Labda kidogo linagusiwa tu kwenye semina za ujasiriamali na mahali pengi yanapofundishwa masomo ya ujasiriamali. Katika ukurasa huu sina nia ya kufafanua sana kwa kina ila tu nitaeleza kwa kifupi maana ya kuwa huru kifedha.

Uhuru wa Kifedha ni nini?

Hii ni hatua ya kiuchumi anayokuwa nayo mtu kiasi kwamba hana shida tena ya fedha maishani mwake.

Ni hatua ya kiuchumi anayokuwa nayo mtu ambapo anakuwa na muda wa kutosha kufurahi na familia yake au watu wake bila kuwa na

wasiwasi wowote wa fedha za matumizi ya kesho.

Uhuru wa Kifedha ni hatua ya kuwa na fedha nyingi zaidi ya matumizi yote ya msingi (basic needs) katika maisha ya kila siku.

Ni hatua katika maisha ambapo mtu anakuwa na Kipato endelevu na kikubwa kuliko matumizi yote. Anakuwa na pesa za ziada baada ya mahitaji yake yote.

Uhuru wa kifedha huleta utulivu wa akili, kisaikolojia na kiroho kutokana na kwamba huna hofu yoyote kuhusu matumizi ya fedha leo, kesho na miaka mingi ijayo hadi watoto wako.

Uhuru wa kifedha ni hatua ya mtu binafsi au taifa kuwa na vyanzo vya mapato vyenye uhakika na visivyotetereka kwa miaka mingi ijayo.

Kupata uhuru wa kisiasa ni jambo zuri kwa kila taifa. Lakini hatua ya wananchi wake kuwa na uhuru wa kifedha ni jambo zuri zaidi ya yote. Kila taifa linapaswa kuhubiri uhuru wa kifedha kwa watu wake.

Uhuru wa kifedha huwafanya watu kuwa na mawazo huru. Wanasiasa pia wanakuwa huru kujiuzuru nyadhifa zao endapo watatakiwa kufanya hivyo kutokana na makosa ya watendaji wao wa chini.

Kinachowafanya waafrika wengi kukataa kujiuzuru wakati mwingine ni kuona kuwa wataathirika kiuchumi na kifedha kwa kuwa nyadhifa walizonazo ndizo huwaletea kipato kikubwa.

Lakini kama mtumishi wa umma amefikia hatua za kuwa huru kifedha hatababaika. Atakuwa huru kufanya maamuzi kwa weledi bila kuogopa kupoteza kibarua chake na kipato chake.

Watu wengi watakuwa wanafanya kazi za umma kwa nia ya kuwatumikia watu na siyo kupata kipato.

Ukiwa huru kifedha huna woga wa maisha. Huna woga wa kufanya uamuzi sahihi kwa kuogopa kupoteza cheo au wadhifa wako.

Uhuru wa kifedha ni suala la kufa na kupona kwa kila mtu kulipigania.

SURA YA 13

Misingi 3 ya Kupata Fedha Bila Jasho

Pamoja na kufafanua miradi inayoleta fedha kwa wingi hapo juu, ni vyema nikafafanua kuhusu misingi kadhaa ya kusimamia ili kuendelea kupata fedha miaka mingi utakayoishi duniani ndugu msomaji.

Ni vyema tukajua kwamba katika kutafuta uhuru wa kifedha hatuna budi kuwa na mifumo au miundombinu ambayo itatuhakikishia kwamba tutimizapo umri fulani tutakuwa huru kabisa.

Ukishaelewa msingi huo huna budi kujifunza mbinu (How) za kupata huo uhuru wa kifedha. Baba zetu akina Mwalimu Nyerere na wenzake walipigania uhuru wa kujitawala kisiasa. Kwa sasa sisi wa leo Tanzania hatuna budi kupambana ili kupata uhuru wa kifedha na kiuchumi sisi na watoto wetu.

Tunapaswa kuelewa kwamba uhuru wa kifedha huleta amani ya moyo wa mtu (peace of mind) na kuishi maisha yenye uhuru wa kweli unaomwezesha mtu kwenda unakotaka, wakati unaoutaka na kulala Hotel unayoitaka duniani.

Ifuatayo ni misingi 3 itakayokuweza kupata uhuru wan a kupata fedha bila jasho kizazi hadi kizazi:

1. Kuwarithisha Nyumba na Mali Watoto

Kwa nini kizazi hiki kina watu maskini sana wa kipato? Jibu la haraka ni kwamba kizazi kilichopita hawakutuachia urithi wa vyanzo vya mapato au mali zinazoweza kubadilishwa kuwa fedha.

Wazazi wetu tuilo wengi walituachia urithi wa elimu au mashamba matupu. Walituachia elimu ya kikoloni ambayo inakutaka uajiriwe tena bila kuwa mbunifu kwa lolote.

Wazazi walituachia mashamba matupu yasiyokuwa na chochote ndani yake. Hali hiyo imetufanya wengi kuendelea kuwa katika mzunguko wa umaskini uliokithiri (Poverty vicious circle) kuanzia mababu zetu hadi sisi wa leo.

Hivyo, Kama tunataka kufuta umaskini kwetu na kwa watoto wetu ili wawe na maisha yasiyo na tatizo la mzunguko wa fedha kwao, lazima tuwarithishe nyumba

na mali kama rasilimali na vitega uchumi vya kifedha vitakavyowawezesha kuwa na mzunguko endelevu wa fedha kutoka kwetu hadi kwa watoto wetu na watoto wao (wajukuu).

Tusipoweka msingi huo umaskini utaendelea kuzunguka kizazi kwenda kizazi. Ifike mahali ambapo watoto wetu hawatahangaikia kujenga nyumba za makazi yao. Wahangaikie vitu vingine vya wakati wao. Siyo kila kizazi kinahangaikia kutafuta ploti kama vile wazazi wao hawakuliona hilo.

Hatuna budi kuelewa kwamba elimu siyo urithi wa watoto ni haki ya watoto wetu. Kama tunaweza kuwahangaikia watoto wetu kupata elimu vivyo hivyo hatuna budi kuwangaikia wapate nyumba na mali na fedha za kuwatosha maisha yao yote.

2. Kupanda Mazao yadumuyo Sana

Msingi huu ni wa muhimu sana kwa faida ya miaka mingi ijayo. Kama nilivyofafanua kwenye sura zilizotangulia ili kupata fedha ambazo haziishi, lazima ukubali kuweka

misingi ambayo italeta fedha mwaka baada ya mwaka.

Kama unataka kuufuta umaskini kwenye familia yako milele na milele, panda mazao yatakayotiririsha fedha miaka 3 hadi 50.

Mazao ya kudumu kama nilivyoyadavua sura zilizotangulia zitakuwezsha kuvuna fedha miaka nenda rudi.

Panda mazao yadumuyo miaka mingikama vile miembe, michikichi, nazi, katani, karafuu, korosho, zabibu, miti ya mbao, n.k. Hakika msingi huo hautavunjika na utabakia historia kwenye ukoo wako.

3. Weka Vitegauchumi Vinavyodumu

Kama unatamani kula bata bila jasho kwa muda mrefu zaidi hakikisha unatumia kipato chako cha sasa kutengeneza vitega uchumi vingi kadri ya uwezo wako. Vitega uchumi au vidaka pesa endelevu vitakuletea fedha kwa kipindi kisichopungua miaka 15 sawa na miezi 180 na kuendelea.

Hebu fikiria ukiwa na vitega uchumi endelevu ukiwa na umri wa miaka 55 au 60 na vitega

uchumi vyako vyote vikawa vinakulipa “Pensheni” kwa miaka yako yote iliyosalia duniani. Kama Mwenyezi Mungu akikupatia umri wa miaka 90 duniani ni raha iliyoje kuishi miaka yote hiyo bila kuwa na mahangaiko ya kipato uzeeni?

Hebu fikiria kulipwa kila mwezi mpaka kufa. Kulipwa na vyanzo vyako vyote shs 3,000,000 kwa mwezi. Kila mwezi bila jasho hadi siku utakapoondoka duniani. Unaonaje msingi huo. Unakaa nyumbani na kila mwezi akaunti yako inasoma. Bila jasho lolote.

SURA YA 14

Una Ndoto Gani Utimizapo miaka 60?

Unaweza kutengeneza ndoto yako na ikatimia utimizapo umri wa miaka 60. Unaweza kutengeneza ndoto yako ya kifedha na kiuchumi miaka ijayo kabla ya kutimiza miaka 60.

Ndoto yakowaweza kuiandika sehemu au ukawa nayo moyoni mwako tu. Epuka kuitangaza ndoto yako kwa kila mtu. Watoto wako waweza kuwashirikisha ndoto yako lakini siyo kila mtu. Kama unaweza kuwa nayo moyoni na ukaisimamia na kufanyia kazi kila wakati itapendeza sana.

Katika semina zangu kwa watumishi wa umma na makanisani ninapoalikwa kufundisha masomo ya kujiandaa kifedha, mmoja wa washiriki wa semina zangu alijibu swali hili akionesha ndoto yake hivi;

“Ndoto yangu kabla ya kutimiza umri wa miaka 60 ni kukamilisha ujenzi waNyumba 10 za Kupangisha zenye vyumba viwili hadi vitatu kila nyumba.

Ndoto yangu ni kwamba nyumbahizozikikamilika zitaweza kuniingizia kipato cha kuanzia shs 2,000,000 hadi 3,000,000 kwa Mwezi kutokana na kodi ya kupangisha.

Pesa ya kujenga nyumba hizo nitaipata kutokana na mshahara wangu wa kila mwezi wa shs 1,500,000 ambapo kila mwezi nitatenga shs 700,000 kwenda kwenye ujenzi wa nyumba na shs 800,000 ndizo pesa nitakuwa natumia kwa mahitaji mengine ya familia kila mwezi”.

Mshiriki wa semina zangu mwingine aliandika hivi; *“Ndoto yangu nikitimiza umri wa miaka 60 ili niwe na uhuru wa kifedha uzeeni nataka niwe na shamba la Miti ya Matunda aina ya embe za Kisasa hekari zipatazo 5 hivi.*

Ndani ya hekari hizo tano napanda miti ya embe ipatayo 500 kwa kila hekari ambapo nitakuwa na jumla ya miti 1000 ya miembe. Matazamio yangu ni kwamba kila mti wa embe utazalisha maembe yasiyopungua embe 200 kwa mwaka miti ikishakomaa vizuri.

Kwa hiyo, nitazalisha embe zipatazo 100,000 kila mwaka. Natarajia kwamba kila embe nitaliuzia shambani kwa shs 300 hadi 500. Kama kila kitu kitakuwa kamandoto yangu ilivyo, ninatarajia

kipato kisichopungua shs 30,000,000 hadi 50,000,000 kwa kila mwaka uzeeni mwangu.

Ili kutimiza ndoto yangu hiyo, kila mwaka ninapanda miti ipatayo 500sawa na hekari moja kila mwaka. Kwa sasa nina umri wa miaka 45 kwa hiyo nikiwa na miaka 50 na kuendelea miembe hiyo ipatayo 2500 itakuwa imekamilika shambani na itakuwa imekomaa kabisa.

Kwa hiyo ndoto yangu ni kwamba nikifika uzeeninitakuwa mzalishaji wa maembe kila mwaka na ninatarajia kuingiza mapato ya fedha yasiyopungua milioni 30 hadi 50 kila mwaka”.

Mshiriki mwingine wa Semina zangu aliandika ndoto yake ya kipato cha uzeeni hivi;

“Nina umri wa miaka 45. Ndoto yangu nikiwa mzee wa miaka 60 nataka niwe na shamba la hekari 12 lenye miti ya mbao aina ya Pinus ipatayo elfu 12. Ili kuweza kutimiza ndoto hiyo, kila mwaka napanda miti 3600 sawa na hekari 3 kila mwaka.

Nitimizapo umri wa miaka 50 miti yote elfu 12 itakuwa imekamilika shambani. Hadi nitakapotimiza umri wa miaka 60 nitakuwa na Shamba lenye miti iliyokomaa na ninatarajia

kuwa shamba la miti ya mbao ambalo litanipatia kipato kisichopungua shs 9,000,000 kwa mwezi kwa kuuza mbao zipatazo 100 tu kila siku kwa bei ya shs 3000 kila ubao sawa na maksio ya mbao 50 za inchi 2 kwa 4 kwa kila mti utakaovunwa.

Ndoto yangu nikuvuna miti 60 kwa mwezi ili kuweza kuvuna miti yote elfu 12 shambani baada ya ya miaka 15 hadi 17. Ndoto yangu ni kwamba kama nitaishi miaka 15 hadi 17 baada ya 60 nitakula pesa hiyo hadi nitimize miaka 75 hadi 77 nikiwa nakula 9000,000 kwa mwezi bila jasho lolote”.

Mshiriki wa semina zangu mwingine alijibu swali hilo kuhusu ndoto yake akisema ifuatavyo;

“Mimi ndoto yangu nitimizapo miaka 60 ni kuwa na Nyumba moja Mjini Kahamaya Kulaza Wageni (Guest House) yenye Vyumba 10 itakayoweza kunilipa takribani shs 6,000,000 kwa mwezi mwezi ambapo nikitoa matumizi yote sitakosa shs 3,000,000 kila mwezi ninazobakiwa nazo mkononi.

Nyumba hiyo ya wageni nitaijenga kidogokidogo kila mwaka kuanzia sasa ambapo nina umri wa miaka 38 ninaamini hadi nitimizapo miaka 50

nitakuwa nimekamilisha ujenzi wa vyumba vyote kumi.

Kila mwezi pesa yoyote ninayopata kuanzia sasa nitaipeleka kwenye ujenzi wa Nyumba hiyo mpaka kieleweke. Naamini nikikamilisha Nyumba hiyo nitakuwa nimejikomboa kifedha na kiuchumi mimi mwenyewe hadi wajukuu zangu.

Nitawaelekeza wanangu jinsi ya kusimamia mapato ya biashara yetu ili hata nikiwa sipo duniani waendeleo kuisimamia na waweze kuishi maisha yenye uchumi imara na bora”.

Hitimisho

Kama una ndoto unayotaka itimie ukiwa na miaka 60 iandike kwenye karatasi au uwe nayo moyoni na uwe unairudia mara kwa mara ili usije ukaisahau.

Je, ndoto yako ni nini ukiwa mzee? Unataka kuwa nakipato cha shilingi ngapi kwa mwezi? Je ni Shs 10,000,000 kwa Mwezi? Je, nishs 3,000,000 kwa mwezi? Weka mikakati utimize ndoto yako ya kifedha.

Andika ndoto hiyo. Ota ndoto itakayokupatia kipato bila jasho maisha yako yote hadi wajukuu wa wajukuu zako.

CHAGUA KUFANYA KAZI HADI KUFA AU KULA BATA HADI KUFA.

KUZEEKEA KAZINI NI CHAGU LAKO.

SURA YA 15

Mithali 60 za Mr. Milinga

Mithali zifuatazo zitakakusaidia kupata hekima ya mafanikio yako unayoyataka maishani mwako. Utafanikiwa kiroho, kimwili, kisaikolojia, kiuchumi na kifedha.

Hakika Mithali hizi zina hekima kubwa ndani yake. Twende pamoja na usome zote ufanikiwe;

- 1) ***NCHI HII SIYO MASKINI, UMASKINI UPO VICHWANI MWA WANANCHI WENYEWE.***
- 2) ***KUPANGA NI KUCHAGUA. CHAGUA MIRADI ITAKAYOKUPA KULA BATA MIAKA MINGI***
- 3) ***MASKINI AKIPATA PESA HUTANUA SANA, TAJIRI YEYE HUTANUAMIRADI YAKE.***
- 4) ***TATIZO SIYO UFINYU WA BAJETI, NI UFINYU WA MAWAZO.***
- 5) ***SHIDA SIYO PESA, SHIDA NI KUTOCHUKUA MAWAZO YA KUPATA PESA.***
- 6) ***UVIVU WA KUFIKIRI NDIYO CHANZO CHA UMASKINI, JARIBU KUWAZA ZAIDI.***
- 7) ***MATENDO YAKO YA KILA SIKU YATAKULETEA UTAJIRI AU UMASKINI.***
- 8) ***UKITAKA KUFUTA UMASIKINI KWENYE UKOO WAKO, PANDA MITI YA KUDUMU.***
- 9) ***WARITHISHE WATOTO NYUMBA NA MASHAMBA, ELIMU NI HAKI YAO.***
- 10) ***ENDELEA KUWAZA KIBILIONEA HATA KAMA HUNA SENTI MFUKONI, UTAJIRI UNAKUJA.***

- 11) WALEE WATOTO WAKO KIMILIONEA NAO HAWATAACHA MALEZI HAYO HADI UZEENI.
- 12) UTAJIRI HAUPATIKANI KIMIJJIZA, NI MIPANGO NA MIKAKATISAHIMI YA MUDA MREFU.
- 13) USIFURAHIE KUPEWA PESA, FURAHIA KUPEWA MBINU ZA KUPATA PESA.
- 14) MAWAZO YA KUPATA PESA NI MATAMU, KUYATEKELEZA SHUBIRI.
- 15) USIPOJITOA KAFARA ILI UFANIKIWE, UTAPATA UFUKARAWA KUKUTOSHA.
- 16) USIFURAHIE KUPEWAMSAADA WA FEDHA, FURAHIA KUVUNA FEDHA.
- 17) WANAOTOA NDIYO WANAPEWA. USIACHE KUTOA KWA WAHITAJI.
- 18) USIMWOMBE MPENZI WAKO PESA, MWOMBE MAWAZO YA KUPATA PESA.
- 19) MAPENZI YA KWELI SI KUPEANA PESA, NI KUPEANA MAWAZO.
- 20) AKUPAYE MBINU ZA KUPATA MAFANIKIO, NDIYE RAFIKI WA KWELI.
- 21) USITAFUTE FEDHA, TAFUTA MAARIFA YA KUPATA FEDHA.
- 22) WENYE MAARIFA MAKUBWA NDIYO WENYE MAFANIKIO MAKUBWA.
- 23) ATAFUTAYE PESA HATAZIPATA, BALI ATAFUTAYEMAARIFA ATAZIPATA.
- 24) USIRIDHIKE NA KUAJIRIWA, TUMIA UJIRAWA AJIRA YAKO KUPATA UTAJIRI.
- 25) KUAJIRIWA SIYO DHAMBI, DHAMBI NI KUZEKAUKIWA MASKINI.
- 26) KUWA MSOMI WA CHUO KIKUU KWAFAA SANA KAMA UNASOMA KILA SIKU.
- 27) WASOMI WASIOSOMA HUFA BILA KUACHA KITU CHA KUSOMWA NA WATU.
- 28) HAKUNA MSOMAJI WA VITABU ALIYEKOSA MAFANIKIO KIFEDHA

- 29) ACHA KUTAZAMA RUNINGA, TAZAMA KITABU CHA ALIYETENGENEZA RUNINGA.
- 30) MATAJIRI HUANDIKA NA KUSOMA VITABU, MASKINIHUKODOA MACHO TU!!
- 31) UWEZO WA KUFANIKIWA UPO KATIKA UBONGO, TUMIA VYEMAUBONGO WAKO.
- 32) HUWEZI KUWA TAJIRI HADI UTAKAPOAMUA KUWA TAJIRI.
- 33) YESU ALIFANYIKA MASKINI DUNIANI, WEWE UWE TAJIRI DUNIANI.
- 34) FEDHA NA DHAHABU NI MALI YA MUNGU, WEKA MIKAKATI MAKINI UTAZIPATA
- 35) MATAJIRI HUSOMA VITABU 50+ KWA MWAKA, MASKINI YEYE HUSHANGAA TU!!!
- 36) HAKUNA ALIYEZALIWA AFE MASKINI. WOTE TUNaweza KUFANIKIWA.
- 37) USIFUATILIE MAMBO YANAYOTOKEA TU, SABABISHA MAMBO KUTOKEA
- 38) UKIONA MAMBO HAYAENDI, NENDA WEWE ACHA MAMBO YAKUFUATE.
- 39) MAMBO HAYAJILETI YENYEWE, HUSABABISHWA KUTOKEA.
- 40) USIPOJIFUNZA UTAKUWA FUNZA. USIPOKWENDA CHUO UTAKUWA CHOO.
- 41) KAMATA SANA MAARIFA MAANA NDIYO UZIMA NA UTAJIRI WAKO.
- 42) USIMTEGEMEE MJOMBA, FANYA KAZI KWA BIDII UTEGEMEWE NA WAJOMBA.
- 43) USIWE TEGEMEZI WA FIKRA, TENGENEZA FEDHAZAKO UTEGEMEWE.
- 44) KUZALIWA MASKINI SIYO KOSA LAKO, LAKINI KUFA MASKINI NDIYO KOSA.
- 45) MATAJIRI HUWEKA MIFUMOENDELEVU YA FEDHA KUMIMINIKA HADI UZEENI, WEWE JE?
- 46) MATAJIRI HUTENGENEZA VYANZO VYA MAPATO ZAIDI YA SABA; WEWE JE?.

- 47) **USISHIRIKI KILA SHEREHE MPAKA NDOTO YAKO YA MAFANIKIO IKITIMIA.**
- 48) **USIPOTENGENEZA VYANZO IMARA VYA FEDHA, UTAFANYA KAZI HADI KUFA.**
- 49) **MAZOEZI YA MWILI YANAFAA SANA, MAZOEZI YA KUWEKA AKIBA YAFAA ZAIDI.**
- 50) **KUCHUKUA MKOPO WA FEDHA KWAFAA KUKIAMBATANA NA MAREJESHO.**
- 51) **KATIKA SAFARI YA MAFANIKIO, USIFE MOYO KABLA YA KUFA MWILI.**
- 52) **USIKATE TAMAA YA KUFANIKIWAKABLA HUJAKATA ROHO YAKO.**
- 53) **NIDHAMU YA FEDHA HULETAUTAJIRI, MATUMIZI HOLELA HULETA UFUKARA.**
- 54) **KUFUNGA NDOA NA MWANAMKE MWEMA NI KUFUNGA MATUMIZI YA HOVYO.**
- 55) **USIPOAMUA KUJIONDOA KATIKA UMASKINI LEO, UTASUBIRI SANA.**
- 56) **MUNGU HAPENDEZWI NA UMASKINI, TUNAJISABABISHIA WENYEWE.**
- 57) **USISOME SANA ILI KUPATA KAZI, SOMA SANA UTATUE MATATIZOYA WENGI.**
- 58) **MAVAZI UVAAYO MBELE ZA WATU, HUASHIRIA UMASKINI AU UTAJIRI WAKO.**
- 59) **UKITATUA MATATIZO YA WATU, FEDHA ZITAKUFUATA KOKOTE ULIPO.**
- 60) **USIJIAMBIE MOYONI, "UZEE UKO MBALI" JIANDAE USIAIBIKE UZEENI.**
- 61) **USIPOJIPANGA VYEMA UJANANI, UZEE UTAKUPANGA KISAWASAWA.**
- 62) **UTAJIRI UDUMUO HUTENGENEZWA POLEPOLE, EPUKA UTAJIRI WA HARAKA.**
- 63) **DUNIA NI KIJIKI, TUMIA WANAKIJIKI WENZAKO KUTENGENEZA FEDHA.**

**64) MABADILIKO HAYAKWEPEKI DUNIANI, BADILISHA FIKRA
ZAKO UFANIKIWE.**

Mwisho

**Kwa mahitaji ya Vitabu vya Mwandishi huyu
wasiliana na:**

- 1) Mr. Milinga (Mwandishi) Simu: 0767285417
- 2) Mrs Regina Milinga 0753455574
- 3) Duka la Vitabu Bukoba (ELCT BUKOBA BOOKSHOP)
- 4) Rugarawa Bookshop Jijini Dodoma (BARABARA YA 8)
- 5) Duka la Vitabu Dar es salaam (Posta-mpya)
- 6) Maduka ya Vitabu Jijini Mwanza, Arusha. Mbeya.

**Kwa mahitaji ya Semina za Elimu ya Fedha
wasiliana nasi kwa: Na. 0767285417; Email:
milinga2016@gmail.com; Twitter: @milinga 2015**